

**MIELEKEO YA WATAWALA WAKUU NA WAHADHIRI WA CHUO KIKUU CHA  
NAIROBI KUHUSU KISWAHILI KAMA LUGHA RASMI NA YA TAIFA NA ATHARI  
ZAKE.**


**MUREA WILSON MBASI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA  
SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI, IDARA YA  
KISWAHILI**

**Julai, 2022**

## UNGAMO

Kazi hii ya tasnifu niyangu mwenyewe na hijawahi tolewa chuoni kingine kutahiniwa kwa mahitaji ya shahada.


Sahihi.....

Tarehe ..03/08/23.....

Murea Wilson Mbasi

Nambari: C50/35763/2019


Tasnifu yetu imewasilishwa ili kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi waliotuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi kupitia idara ya Kiswahili.

Sahihi.....

Tarehe ..03/08/23.....

Dkt. Jefwa Mweri

(Msimamizi)

Sahihi.....

Tarehe ..17/08/2023.....

Dkt. Ayub Mukhwana

(Msimamizi)

## **TABARUKU**

Nawatabarukia kazi hii: Baba yangu Joseph Murea, mamangu Jerusha Mwonjiru, Germano Mutegi, Esther Mukubu, mke wangu mpendwa Joy Karambu Mbasi, mtoto wangu Gian Shamsi Mbasi na ndugu zangu wote.

## SHUKRANI

Natoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, nguvu, ujuzi na kuniwezesha kukamilisha kazi hii.

Pasi na changamoto nyingi, ukarimu, watu walituauni sana kufaulisha kazi yetu. Kwa walezi ambao ni wasimamizi wangu Shukrani ziwaendee wote Dkt. Jefwa Mweri na Dkt. Ayub Mukhwana kwa malezi mema, ushauri na kunielekeza kuifanya tasnifu hii. Ustahimilifu wao wa kitaaluma umenifaa katika sna. Maulana awaongeze busara zaidi, waishi miaka na mikaka watambulise tarumbeta za halafu.

Ninawashukuru walimu wengine ambao ni wahadhiri walioweza kunishauri mpaka nikamaliza kazi hii. Shukrani kwa Prof. Iribe Mwangi, Prof. John Habwe, Prof. Kyalo Wamitila, Prof. Mwenda Mbatia, Prof. Kinene wa Mutiso, Prof. Evans Mbuthia, Dkt. Prisca Jerono, Dkt. Zaja Omboga na Dkt. Hannah Mwaliwa.

Nawashukuru babangu Joseph Murea na mamangu Jerusha Mwonjiru na ndugu zangu wote kwa nafasi waliyoichukua kuniongoza kunitia moyo mpaka mwisho kazi hii. Mungu awakumbuke Kwa kila hali

Shukrani za dhati Kwa mke wangu Joy Karambu kwa kusimama nami kwa njia zote na kunivumilia mpaka mwisho.

Nawashukuru wanafunzi wenzangu tuliosoma nao Kwa kunitia motisha kukabiliana na changamoto katika kozi hii. Maulana awabariki Jerusha Mbathi, Mark Otiende, Janet Kemunto Na Cindy Wanjiru. Vilevile siwasahau marafiki wa karibu walionitia motisha ambao walinitangulia katika safari hii. Shukrani zangu ziwaendee Daniel Nyamboga, Nicholus Makanji na marafiki wote wakiwemo Frankline Muthaura, Frankline Kiambi na Germano Kairira.

Shukrani kwamarafiki ambao sijawataja. Mchango wao ni ulichangia pakuwa katika kazi hii. Shukrani sana

## **IKISIRI**

Tasnifu hii ni utafiti wa mielekeo ya wakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa. Mielekeo yao inatarajiwa kuwaongoza wapangaji wa sera ya lugha ili kubuni njia na mbinu za utekelezaji wa majukumu rasmi na kukipa Kiswahili nafasi yake katika utekelezaji wa majukumu rasmi na ya kitaifa. Utafiti wa kina ulifanywa nyanjani tulipopata data msingi tuliyoikusanya kwa kutumia hojaji, utazanaji wa wahojiwa na mahojiano kubaini namna wanavyotumia Kiswahili, kikiwemo Kiingereza pamoja na lugha zingine chuoni ili kujua masiala yanayosababisha mielekeo iliyopelekea kuondolewa kwa Idara ya Kiswahili chuoni. Kulingana na matokeo ya utafiti huu, watafitiwa walibainisha kuwa wanafahamu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa lakini urasimi wa Kiswahili katika utekelezaji wa majukumu rasmi haujatambuliwa. Mielekeo ya watafitiwa kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa imetokana na masiala ya kiisimu, kihistoria, kiuchumi na kijamii. Katika uchanganuzi wa data tuliongozwa na nadharia ya makutano na mwachano ya Giles (1982)

## **Ufafanuzi wa istilahi**

**Wakuu** – Watu wenye madaraka juu ya wengine mahali pa kazi/viongozi wa wengine kazini (chuoni)

**Wahadhiri** – Walimu wanaofundisha chuoni

**Lugha rasmi** – Lugha itumiwayo katika mawada rasmi kama bungeni.

**Lugha ya taifa** – Lugha iliyoteuliwa katika taifa ili itumike katika mawasiliano na wananchi

**Wingilugha** – Uwezo wa kuwa na zaidi ya lugha moja kutumika eneo fulani

**Sera ya lugha** – Ni maamuzi ya kisheria na kiutawala yanayofanywa kuhusu lugha.

**Hadhi** – Ni heshima na cheo inayopewa lugha kutokana na majukumu inayotekeleza.

**Mielekeo** – Ni hisia ambazo watu hudhihirisha wanapokuwa katika hali zinazohitaji kufanywa uteuzi wa kitu au jambo kati ya mambo au vitu vingi. fulani. Hali hizi huonyesha ukubalifu wa mtu kuhusiana na kitu fulani. Ni hali inayodhihirisha mitazamo ya ndani inayohusiana na mambo fulani.

**Mielekeo chanya** – Ni hali inayodhihirisha hali ya mtu kuwa na mtazamo mwema wa kupenda kitu fulani

**Mielekeo hasi** – Ni hali inayodhihirisha kutopenda jambo au kitu fulani.

**Makutano** – Hali ambapo watu wawili au Zaidi, vitu, jambo au hali kukongamana pamoja

**Mwachano** – Hali ya kutengana kwa watu, vitu, hali au jambo

## YALIYOMO

UNGAMO.....	<b>Error! Bookmark not defined.</b>
TABARUKU .....	iii
SHUKRANI.....	iv
IKISIRI .....	v
Ufafanuzi wa istilahi.....	vi
SURA YA KWANZA .....	1
1.0 Utangulizi .....	1
1.1 Usuli wa mada.....	1
1.2 Tatizo la utafiti .....	5
1.3 Malengo na madhumuni ya utafiti .....	6
1.4 Maswali ya utafiti.....	6
1.5 Sababu za kuchagua mada.....	7
1.6 Upeo na mipaka.....	8
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada .....	9
1.8 Misingi ya kinadharia.....	12
1.8.1 Nadharia ya makutano na mwachano.....	12
1.9 Mbinu za utafiti .....	14
1.9.1 Mbinu za ukusanyaji data .....	15
1.9.2 Mbinu za uchanganuzi wa data .....	17
1.9.3 Uwasilishaji wa data.....	17
SURA YA PILI.....	19
2.0 HISTORIA YA MIELEKEO YA KISWAHILI NCHINI KENYA .....	19
2.1 Utangulizi .....	19

2.2 Kipindi cha ukoloni.....	19
2.2.1 Kabla ya vita kuu ya pili ya dunia .....	19
2.2.2 Wakati wa vita kuu ya pili ya dunia .....	21
2.2.3 Baada ya vita kuu ya pili ya dunia.....	22
2.2.4 Baada ya Ukoloni .....	25
2.2.5 Sekta ya elimu .....	28
2.2.6 Vyombo vya habari .....	30
2.2.7 Hitimisho .....	31
SURA YA TATU .....	32
3.0 MIELEKEO YA WAKUU NA WAHADHIRI WA CHUO KIKUU CHA NAIROBI KUHUSU KISWAHILI .....	32
3.1 Utangulizi .....	32
3.1.1 Matokeo ya Utafiti.....	33
3.1.2 Mielekeo ya wakuu na wahadhiri.....	37
3.1.3 Mielekeo ya Wasimamizi wakuu .....	42
3.1.4 Hitimisho.....	46
SURA YA NNE.....	47
4.0 MASWALA YANAYOSABABISHA MIELEKEO KUHUSU KISWAHILI NA ATHARI ZAKE .....	47
4.1 Utangulizi .....	47
4.2. Athari za mielekeo ya watawala wakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa. ....	58
4.3 Hitimisho.....	60
SURA YA TANO .....	62
5.0 Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo .....	62



5.1 Utangulizi .....	62
5.2 Muhtasari wa utafiti .....	62
5.3 Changamoto za utafiti .....	63
5.4 Mahitimisho .....	64
5.5 Mapendekezo .....	65
MAREJELEO .....	66

Kielelezo 1: Upendeleo wa Lugha ya Kujaza Hojaji wa wahadhiri na watawalawakuu.....	34
Kielelezo 2 : Lugha ya Kujaza Hojaji kiumri .....	35
Kielelezo 3: Matumizi ya Kiswahili kama Lugha Rasmi .....	39
Kielelezo 4: Matumizi ya Kiswahili Kiumri.....	40
Kielelezo 5: Kipengele cha kitengo cha elimu .....	41
Kielelezo 6: Mielekeo ya watawala wakuu wa Chuo kuhusu kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa .....	43

Chati 2 .Uchanganuzi wa data ya walengwa. ....	36
--	----

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

#### 1.1 Usuli wa mada

Kiswahili kina majukumu mengi ya kutekeleza katika utekelezaji na kushughulikia mambo ya kiuchumi, kisiasa na hata kielimu. Ili kufaulisha hali hii ya kukikuza, kuimarisha na kukiendeleza Kiswahili, sera ya lugha nchini Kenya ilisaidia pakubwa katika nafasi hii. Sera ya lugha huwa ni maamuzi ya kisheria na kiutawala yanayofanywa kuhusu lugha. Huwa ni mipangilio ya kiserikali inayohusu namna lugha inavyotumiwa katika nchi. Mbaabu (1996) asema kuwa sera ya lugha ni sera ya umma. Hii ni nkwa sababu ni kipengee mojawapo cha mpango-lugha Mekacha (2011). Kwa hivyo huchukuliwa Kama jumla ya sheria, matamko, mawazo, taratibu Na kanuni zinazoeleza taratibu za utekelezaji mabadiliko na lugha inavyotumiwa katika jamii. Sera ya lugha hutumiwa kuelekeza masuala utawala, za kielimu na hata vyombo vya habari katika nchi ya nchini Kenya.

Kiswahili kimekuwa kikitumiwa kutekeleza majukumu ya lugha ya taifa mpaka 2010 katiba ya Kenya ilipokipa hadhi mpya ya kuwa lugha rasmi. Ijapokuwa, katika hali za kukitumia Kiswahilihakina hadhi hiyo kwani tukikiangalia kinavyotumiwa katika mianda rasmi hakitumiki kutekeleza majukumu rasmi kama vile kuandika barua rasmi, kuandika vyeti vya kufa na kuzaliwa, kuandikia paspoti na mengine rasmi mingineyo. Kiswahilikimepitia mabadiliko mengi tangu ukoloni. kwa mfano, mwaka wa 1969 Mzee Jomo Kenyatta alikuwa amesema kwamba Kiswahili kikuzwe na kiwe lugha rasmi na kitumiwe bungeni katika uendeleshaji wa shughuli za bunge. Wakati huo watu walionekana kutoridhika na wengi walipinga wakidai kuwa Kiswahilihakikuwa kimejitoshelesha kimisamiati ya kisayansi pamoja na ya kiufundi. Kwa hivyo hakingefaa kutumiwa kama lugha rasmi ya taifa la Kenya. Kuna njia zilizotokana na ripoti za tume hizi zilizotumiwa kukipa Kiswahili na kuonyesha nafasi yake katika matumizi.

Ripoti hizi ni kama vile ripoti ya Ominde (1964). Ripoti hii ilionyesha kuwa Kiswahilikama lugha ya kutumiwa kuunganisha watu katika taifa na lingua franka ya mawasiliano barani Afrika. Ripoti ya tume ya Gachathi (1976) - ilipendekeza Kiswahili kufunzwa likiwa la lazima katika shule za msingi na hata za upili.

Tume ya Mackay 1981-Ilitoa mapendekezo yaliyoibua mfumo uliokuwepo wa elimu ya (8.4.4) na kuleta mabadiliko makuu katika lugha ya Kiswahili kwa shule za upili. Mapendekezo ya tume hii yalilenga kuwafaa wanafunzi kwa kuwapa mafunzo ambayo yangewafaa hata baada ya shule kupigana na kukabiliana na mambo mengine katika maisha. Ripoti ya tume hii vilvile ilipendekeza kuanzishwa chuo kingine ili Kiswahili kifundishwe chuoni humo. Vilevile Kiswahili kiwe cha lazima shule za upili na za msingi na kitahiniwe katika mtihani wa kitaifa (Mbatiah 2012). Mapendekezo haya yalileta kuanzishwa chuo kingine kikuu cha Moi cha pili nchini Kenya kikiwa na idara ya Kiswahili 1987.

Kufikia mwaka wa 1985, silabasi ya Kiswahili nayo ilisisitiza kufundishwa stadi za kusikiliza na kuzungumza zisizokuwa zikitahiniwahapo mbeleni zikitiliwa maanani. Katika Wakati huo foni zilizokuwa na utata kuzitamka zilisisitizwa ili kuimarisha matamshi.

Katika mwaka wa 2002 vipindi wa Kiswahili navyo viliongezwa katika vitengo vya shule za msingi kutoka vipindi vitano mpaka vipindi sita. Hali iliyotokana na mapitio ya mtaala wa Kiswahili uliofanywa ngeli za Kiswahili ambazo ni pembejeo katika sarufi ya Kiswahili zikilengwa (Mbaabu 1995).

Katiba ya Kenya 2010 ikakikuzi na kukipandishia hadhi kuwa lugha rasmi na ya taifa kwa kutekeleza majukumu na kuendeleza shughuli bungeni, mahakamani na za kisiasa. Kwa mfano Katika katiba ya Kenya ya 2010 sura ya pili (2) ibara ya saba (7) kutoka sehemu ya kwanza mpaka ya tatu (1-3), Kiswahili kama kilivyo Kiingereza kilipewa nafasi ya kutekeleza wajibu wa lugha rasmi. Kama lugha ya kiasili, katiba inatekeleza kauli zake za kuendeleza, kulinda, kukuza na kuzitumia lugha za kiasili pamoja na lugha ishara na breli kwa kuzipa nafasi katika mawaailiano kutumika kutekeleza majukumu katika jamii.

Lakini hata baada ya mabadiliko kufanywa. Nafasi ya sera ya lugha ya kukikuzi na kukipa Kiswahilinafasi katika kutekeleza majukumu rasmi haijatambuliwa. Hii ni kwa sababu bado kuna watu wanakichukulia Kiswahili kama lugha ya chini. Kwa mfano, Kiswahili hakijatumiwa kwa kina na wanasiasa bungeni. Pia baadhi ya shule za sekondari na za msingi humu mchini, watafiti wa awali kama vile Mirianga (2014) anasema kuwa Kiingereza kimepewa siku nyingi za kukizungumza kuliko Kiswahili. Wanafunzi wengi katika vyo vikuu hasa wale wanaotaalamikia Kiswahili pia mara nyingi hawapendi kuwasiliana kwa Kiswahili kwa Kiingereza. Hii inaonyesha

kwamba Kiswahilikina hukuliwa kama lugha isiyo na maana sana ikilinganishwa na lugha zisizokuwa za kiasili kama Kiingereza.

Janbo hili la kukiona Kiswahili kuwa lugha duni inadhihirika hata kwa viongozi wa serikali. Kwa mfano katika siku ya kuadhimisha sherehe za madaraka tarehe 01/06/2015, Rais Uhuru Kenyatta alihutubu hotuba yake kwa mwida mwingi kwa Kiingereza mpaka wanataifa wakamwambia atumie Kiswahili. Hii inaonesha kwamba Kiswahili hakishughulikiwi kama lugha rasmi. Mirianga (2014) ansema kuwa Kiswahili kupandishwa hadhi ya kuwa lugha rasmi kutasaindia Kiingereza kutekeleza majukumu rasmi katika mianda rasmi tofauti. Kudunishwa huku kunaonyesha kuwa Kiswahili kama lugha rasmi hakijamea mizizi katika hadhi yake kutekeleza majukumu rasmi. Huu ndio msukumo unaoibua chanzo cha utafiti wetu.

Umilisi na utendaji wa Kiswahili basi hutegemea kinakotumiwa, kinakofundishwa na mielekeo ya wanaofundisha. Kwa hivyo kukua na kuendelea kwa Kiswahili hutegemea na huwahusu walimu na hata watafiti Babusa (2010) na Mwihaki (2006). Kwa sababu hii ni muhimu kuwachunguza wasomi ambao ni wakufunzi na watafiti wa ngazi za juu. Kwa kufanya hivi ili tutambua mielekeo yao kuhusiana na Kiswahili na utenda kazi wake kama lugha rasmi na ya taifa kwa sababu wao ndio hufanya tafiti za kina zinazoaminika. Vilevile, hata baada ya kufanya tafiti zao wao huchukuliwa na kufanya kazi na mashirika ya kimataifa wanakotumika na UNESCO kuendelea Kiswahili.

Mielekeo ya wakuu na wahadhiri hawa itatoa picha halisi kuhusu mambo yaliyoko kwenye katiba yanayozungumzia Kiswahili na kwa hali hiyo tunaweza kusema kwamba lugha haiwezi kupangwa kama vile wanasisia wametupangia lugha na kufanya Kiswahili kuwa lugha ya taifa ya kwanza. Mielekeo yao pia itabainisha iwapo lugha inaweza kupangwa au la na kuwakumbusha wapangaji lugha kwamba kufanya utafiti kuhusu lugha ni muhimu ili kupata maoni ya watu kabla ya kutia chochote kinachohusiana na lugha katika katiba. Mielekeo yao hatimaye itajaza pengo la kiakademia na kuwasaidia wapangaji lugha kuimarisha lugha na lugha nayo itaendelea kupiga hatua mbele.

Tutawatafiti wakuu na wahadhiri wa chuo kikuu ambao ni nguzo muhimu katika utekelezaji wa majukumu rasmi na yasiyo rasmi kwa kutumia lugha tofauti katika miktadha tofauti. Aidha wana tajriba kubwa ya matumizi ya lugha katika mawanda mapana ya kielimu, kufundisha

vyuoni,uandishi,uhariri,katika vyombo vya habari,mtandaoni,katika tafsiri nje ya mawanda rasmi ya kitaifa na kimataifa.Wakuu hawa na wahadhiri tunaolenga kuchunguza uheshimiwa na kuaminiwa kwa tajriba yao kuhusu lugha inavyotumiwa.Maoni yao kuhusu matumizi ya lugha katika utekelezaji wa majukumu rasmi na yasiyokuwa rasmi basi yataonyesha mielekeo yao kuhusu Kiswahilina majukumu yanayotekelezwa na lugha hii.

Kiingereza kilitangulia Kiswahili kuwa lugha rasmi. Hivyo Katiba ya Kenya kukipa Kiswahili jukumu hilo linaweza kuwa swala ambalo limeibua mitazamo tofauti kati ya watumiaji wengi wa lugha hii haswa wale waliobobea na kuitaalamikia lugha ya Kiswahili.Nabea (2009) anasema kwamba ni asilimia ndogo sana ya wananchi wanaofahamu Kiingereza. Anasisitiza kuwa takriban asilimia ishirini na tano(25) tu ya wananchi ndiyo ina uwezo wa kuifahamu lugha ya Kiingereza.Hata hivyo pasi na kuwa ni lugha inayoeleweka na wachache , anasema ndiyo lugha inayomiliki mawada rasmi na kutawala huku ikipewa mamlaka ya hadhi ya hali ya juu kuliko lugha zingine.Katika hali tumizi, Kiingereza kimekuwa kikitumiwa kama lugha ya ufundishaji rasmi ilhali lugha za kienyeji kama kilivyo Kiswahili kikitumika kama lugha ya taifa tu.Maoni ya wahadhiri kama vile Mukhwana(2008) na King'ei(2010) ni kwamba tangu enzi za ukoloni,sera ya lugha imekuwa imekumbatwa na matatizo anuwai hususan kutoka(1895-1963).Wana maoni kuwa Kiingereza kimekuzwa na kupewa hadhi ya juu kuliko lugha zingine mpaka kikazitinga hasa Kiswahili.Hii ni hali ambayo imewafanya wanajamii kuwa na mielekeo hasi kuhusiana na lugha za kiasili kama Kiswahili huku wakijenga mielekeo chanya kwa lugha za kimagharibi kama vile Kiingereza. Lugha za kiasili kama kilivyo Kiswahili zina manufaa kwa sababu kila lugha ina nafasi yake hasa katika mashiko ya traiglosia. Kwa hivyo kwa kuwa kila lugha hutekeleza majukumu yake haipaswi kupuuziliwa hivyo kila lugha ni muhimu.

Kutokana na mielekeo ya aina hii kuna watu katika baadhi ya jamii hawawezi kutamka hata sentensi moja ya Kiswahili mambo ambayo hayakutiliwa maanani na wizara ya elimu lakini baada ya kuwa lugha rasmi tuna imani itatumika katika mianda rasmi ikiwemo ile ya elimu.Wanajamii wanakichukulia Kiingereza kama lugha bora zaidi ikilinganishwa na lugha zingine hali ambayo imesababisha kuzidunisha na kuzididimiza.Mitazamo ya wanajamii ni kwamba elimu bora ni kama ngazi ya kufikia maisha bora na vilevile ajira nzuri mukhwana(2008:2).Hii imetokana na hali kwamba kutoka wakati wa ukoloni,Kiingereza kama lugha ya kikoloni kilinasibishwa na kuhusishwa na elimu bora na wakoloni.

Kulingana na Mohochi (2011),Kiswahili kimedharauliwa.Anatoa mfano kwamba katika majarida yanayoandikwa na kutolewa hapa nchini Kenya ambayo huwa na mada tofauti,ni machache mno kwa mfano majarida saba tu huandikwa kwa Kiswahilikati ya majarida thelathini na matatu(33).Hii ni hali ya kukibeza Kiswahilina kukididimiza ambayo inasababisha mielekeo hasi kuhusu kiswahili.Kutokana na hali hii Kiswahili kupewa nafasi ya kutekeleza majukumu rasmi kunatarajiwa kuwa kumeibua mielekeo fulani kwa wakuu na wahadhiri wa vyuo vikuu. kulingana na kinavyotekeleza wajibu huu pamoja na Kiingereza kama lugha zote mbili rasmi. Mielekeo hii ya wakuu na wakufunzi wa chuo kikuu haijakuwa ikitiliwa maanani. Kwa sababu hii utafiti huu utatafiti mielekeo ya wakuu na wakufunzi wa chuo kikuu cha Nairobi ili kugudua ukubalifu wao kuhusu hadhi iliyopewa Kiswahilikama lugha rasmi na ya taifa na athari zake.

## **1.2 Tatizo la utafiti**

Kiswahilini lugha ya kwanza rasmi tena ya taifa humu nchini Kenya.Lugha hii ina manufaa anuwai katika kuendeleza shughuli za kila siku kama za kibiashara, kiuchumi na kielimu. Kiswahili kimekuwa chombo imara cha kuunganisha wakenya na kuwahamasisha katika shughuli za kisiasa kwa kutumia ujumbe wa msamaha, amani na ushirikiano. Hutumiwa kuhifadhi historia ya jamuhuri na shughuli za jamii mbali mbali za wa Kenya kwa kizazi kijacho.

Vyuo vikuu ni taasisi muhimu katika ukuzaji na uendelezaji lugha kikiwemo Kiswahili.Vyuo vikuu ndizo taasisi za upeo zinazoshughulikia masuala ya elimu,usomi,ufundishaji,umilisi,utendaji na utafiti wa masuala ya lugha kote ulimwenguni.Kwa hivyo washikadau wakuu katika vyuo vikuu wanaoendeleza shughuli hizi ni wakuu na wahadhiri wa chuo.Kutokana na hadhi ya Kiswahili nchini Kenya,tunatarajia kwamba wakuu wa chuo wamekipa majukumu mengi katika mawasiliano rasmi kama vile,uandikaji wa vyeti rasmi kwa Kiswahi lina mihadhara kutolewa kwa Kiswahili. Vilevile ikiwa ya kwanza rasmi naya taifa, tunatarajia kwamba mbali na wakufunzi wa lugha, wakuu na wahadhiri wa idara zingine katika chuo kikuu cha Nairobi watakuwa na mchango mkubwa katika kukikuza na kukiendeleza Kiswahili. Hata baada ya kupewa hadhi ya lugha rasmi ya kwanza na lugha ya taifa, mabadiliko haya katika sera ya lugha ya kukikuza na kukipa Kiswahili nafasi katika kutekeleza majukumu rasmi bado kuna watu wanaokiona Kiswahi lini lugha ya chini. Tafiti za awali zinaonyesha kwamba wengi wa wakufunzi katika vyuo vikuu hudhalilisha Kiswahili.

Wakuu wa chuo na wakufunzi wengi katika vyuo vikuu huonekana kupendelea kutumia Kiingereza zaidi. Hii huonyesha kuwa Kiswahili ni lugha isiyo na maana sana na kwamba Kiingereza ndicho muhimu zaidi. Kudunishwa huku kunaonyesha kuwa Kiswahili kama lugha rasmi hakijamea mizizi katika hadhi yake kutekeleza majukumu rasmi. Aidha kunaweza kuwa kiini cha jaribio la kuchomolewa kwa idara ya Kiswahili na kupelekwa katika idara ya lugha. Hiki ndicho kiini cha utafiti wetu. Kwa sababu hii tutatafiti mielekeo ya wakuu na wahadhiri wa chuo kikuu cha Nairobi ili kugudua ukubalifu wao kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa.

### **1.3 Malengo na madhumuni ya utafiti**

Lengo kuu la utafiti wetu ni kuwatafiti wakuu na wakufunzi wa chuo kikuu cha Nairobi ili kugudua ukubalifu wao kuhusu majukumu yaliyopewa lugha hii kutekeleza wajibu rasmi na wa kitaifa. Ili kufaulisha lengo letu tutaongozwa na madhumuni haya:

- i. Kutafiti mielekeo ya wakuu wa Chuo Kikuu cha Nairobi kuhusu hadhi ya lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa.
- ii. Kutafiti mielekeo ya wahadhiri wa chuo kikuu cha Nairobi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na lugha ya taifa.
- iii. Kutafiti athari za mielekeo hii ya wakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi kuhusu kukitumia Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.
- iv. Kubaini iwapo lugha ya Kiswahili imeweza kutekeleza majukumu yake katika mianda rasmi katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

### **1.4 Maswali ya utafiti**

- i) Je, wakuu wa Chuo Kikuu cha Nairobi wana mielekeo ipi kuhusu hadhi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa?
- ii) Je, wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi wana mielekeo ipi kuhusu Kiswahili kamalugha rasmi na lugha ya taifa?
- iii) Je, mielekeo hii ina athari gani katika kukitumia Kiswahili katika Chuo hiki?
- iv) Je, Kiswahili kimeweza kutekeleza majukumu yake katika mianda rasmi katika Chuo Kikuu cha Nairobi?

### **1.5 Sababu za kuchagua mada**

Tafiti kadha zinazohusu mielekeo ya kijamii na masuala la lugha nchini Kenya lakini hakuna utafiti uliofanywa ukiangazia mielekeo ya wakuu na wahadhiri wa vyuo vikuu kuhusu Kiswahilikama lugha rasmi na ya taifa. Katiba ya taifa la Kenya ya 2010, iliongezea Kiswahilihadhi mpya ya kutekeleza majukumu rasmi sawa na Kiingereza.Hali hii ni tofauti na matarajio ya waKenya kulingana na katiba ya Kenya ya 2010. Hii ni kwa sababu baadhi ya majukumu lugha hii ilipewa kutekeleza haitekelezi kwa mfano uandishi wa barua rasmi .Hali hii ilitupa motisha ya kutafiti mielekeo ya wakuu na wahadhiri wa chuo kikuu cha Nairobi nchini Kenya kuhusiana na suala hili,namna mielekeo hii inavyoweza kusaidia utekelezaji wa majukumu kwa lugha asilia,hali ya matumizi ya Kiswahi lina Kiingereza kama lugha rasmi na iwapo wakuu na wahadhiri wanakienzi Kiswahili kama lugha rasmi.Utafiti utatueleza kama Kiswahili kinatekeleza majukumu ya lugha rasmi kama kinavyotarajiwa kutokana na kauli za katiba ya Kenya ya 2010.

Vyuo vikuu huwa ni taasisi muhimu sana katika ukuzaji, uendelezaji na utekelezaji wa lugha katika taifa. Tutajikita katika Chuo Kikuu cha Nairobi.Chuo hiki kinapatikana jijini Nairobi. Wahadhiri wa vyuo vikuu ndio washikadau wa msingi katika matumizi ya lugha kwa njia tofauti na mazingira tofauti hasa wao huhusika pakubwa katika tafiti zinazo changia sera ya lugha nchini. Wakuu na Wahadhiri hawa wana tajriba kubwa sana katika utekelezaji wa maswala ya elimu hapa nchini Kenya ndio waliofikia upeo wa juu zaidi katika utoaji wa maamuzi ya matumizi ya lugha na masomo mbalimbali. Pia wao hufanya kazi na mashirika ya kimataifa na hasa UNESCO kuendeleza Kiswahili.Kwa hivyo wanayoshikilia kuhusu utekelezaji wa maswala ya lugha hayawezi kupuuzwa. Hivyo mielekeo yao kuhusu suala hili itatusaidia kufahamu uhusika wao, michango na ukubalifu wao kuhusu Kiswahilikama lugha rasmi na ya taifa na utekelezaji wa majukumu rasmi kuhusiana na Kiswahilina Kiingereza.

Mielekeo ya lugha huathiri hadhi yake. Kwa upande mwingine, hadhi ya lugha, matumizi na uendelezaji wake Holmes (1992). Basi mielekeo ya watafitiwa tunaolenga kuhusu suala hili itaonesha athari na itasaidia washikadau katika sekta ya elimu kuboresha na kuendeleza Kiswahili kama lugha rasmi katika hali tumizi ya lugha hii.Matokeo ya utafiti huu yatakuwa msingi wa kutolea mapendekezo ya kuimarisha lugha kati ya watafiti na wasomi.Matokeo ya mielekeo ya watafitiwa itatumiwa na wanasera na wapangaji wa lugha nchini Kenya kujaza pengo la



kiakademia na kukipa Kiswahili nafasi yake katika utekelezwaji wa majukumu rasmi katika sekta na taasisi tofauti nchini. Utafiti huu utatoa mwanga wa utekelezwaji wa majukumu rasmi kwa kutumia lugha zote mbili; Kiswahili na Kiingereza kwa usawa katika mazingira mbalimbali. Vilevile ripoti ya utafiti wetu itachangia pakubwa kwa kazi za kimaandishi ya kitaaluma yatakayohusu mielekeo katika jamii ya wingilugha ya Kenya.

Matokeo ya utafiti huu yatasaidia wanaofundisha lugha na isimu jamii kwa jumla kukabiliana na visababishi vya mielekeo hasi ambavyo huathiri ufundishwaji wa lugha hapa nchini. Mwisho kutokana na matokeo ya wataalamu tunaoenda kuwatafiti, Kiswahili kitaundiwa mikakati ya kuhakikisha kuwa kinatekeleza majukumu rasmi bila ubaguzi au maonevu katika baadhi ya miktadha kama inavyotarajiwa kulingana na katiba ya taifa la Kenya ya 2010.

Hivyo kutokana na utafiti huu, kama matokeo ya mielekeo ya watafitiwa itakuwa chanya tutazingatia mbinu mwafaka za kuboresha utendakazi wa Kiswahili uwe bora zaidi na iwapo matokeo yatakuwa hasi basi mikakati bora itabuniwa ili kuimarisha utendakazi wake katika miktadha rasmi.

### **1.6 Upeo na mipaka**

Katika utafiti wetu tutatafiti mielekeo ya wakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa. Tutachagua kushirikisha wahadhiri wa chuo kikuu cha Nairobi kwa sababu, chuo hiki kimo katikati mwa jiji la Nairobi na mji mkuu wa Kenya ambapo lugha rasmi na lugha ya taifa hutumika kwa kiasi kikubwa mikutanoni na katika mawanda mengine rasmi. Chuo hiki kama kinavyojulikana ndicho chuo kizee zaidi hapa nchini kinachoaminika kuzaa vyuo vingine vingi vinavyoshughulikia maswala ya utafiti na ufundishaji wa wa masomo mbalimbali nchini Kenya. Chuo hiki kina wakuu na wahadhiri wengi Maprofesa na Madaktari wanaotafiti na kufundisha lugha na masomo mengine. Baadhi yao ni wa kutoka nje ya taifa la Kenya. Pia kuna wanafunzi wengi wa kutoka vyuo vingine nje ya Kenya wanaoshughulikia na kutafiti kuhusu lugha na masomo mengine katika idara mbalimbali kama vile Kiingereza, Kikorea na Kichina.

Wakuu na wahadhiri hawa baadhi yao ni Wataalamu ambao ni magwiji katika uteuzi, matumizi na utekelezaji wa majukumu ya lugha katika miktadha rasmi na isiyo rasmi. Kwa hivyo inatarajiwa kuwa mielekeo yao kuhusiana na suala hili itakisi mielekeo ya wahadhiri wengine wote wa vyuo

vikuu nchini Kenya. Tutajifunga kwa wakuu kama vile: Sansela, naibu sansela, wenye viti wa baraza, maseneta, wenye viti wa idara mbalimbali na wasajili wa akademia. Kuwatafiti wakuu hawa kutatusaidia kwasa babu wao ndio hufanya maamuzi ya utekelezaji wa majukumu muhimu chuoni.

Vilevile tutawatafiti wahadhiri wanaofundisha masomo mbalimbali pamoja na wahadhiri wa idara za lugha kama vile Kiingereza, kichina, kikorea na kijapani ili tupate maoni yao kuhusu Kiswahilikama lugha rasmi na ya taifa. Idara hizi ni muhimu kwetu kwa sababu zote hushughulikia maswala ya lugha na zote hujenga nyumba moja ambayo ni lugha. Kwa hivyo kuna uwezekano kuhudumu mafanikio ya lugha

Wakuu na Wahadhiri wa jinsia zote mbili ya kiume na ya kike watahusishwa katika utafiti. Wakuu na Wahadhiri wa chuo kama tujuavyo ni wataalamu wakuu na vigogo wa kuigwa na watumiaji wa lugha hasa wapangaji na wahusika katika sera ya lugha nchini. Hivyo wakuu na wahadhiri wa tutakao watafiti kama wawakilishi, tunatarajia kuwa majibu, maoni, mitazamo na mielekeo yao kuhusu suala hili itatoa picha kamili itakayowakilisha na kuakisi mielekeo ya wakuu na wahadhiri wa vyuo vikuu vingine vyote nchini Kenya.

### **1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada**

Kiswahili kina majukumi ainati ya kutekeleza kiutawala, ya kijamii, ya kielimu, kisiasa na hata ya kiuchumi. Limekuwa somo la kufundisha na kiufundishwa vya vyuo na hata katika vitengo vingine vya kielimu na hata kutahiniwa katika mitihani ya kitaifa katika vitengo vya shule za msingi na zile za upili. Kwa hivyo tafiti nyingi zimefanywa kuhusiana na suala la mielekeo hasa ikilenga masuala ya kielimu na namna Kiswahili kinavyotekeleza wajibu wake katika Nyanja tofauti. Mielekeo si suala geni kwa kuwa limeshughulikiwa katika tafiti nyingi katika vitengo kama vile vya shule za msingi na za upili katika maeneo tofauti ya taifa la Kenya. Mielekeo imefanya kwa kuangazia walimu na wanafunzi wa shule za msingi na za upili kuhusu Kiswahilikama lugha rasmi lakini hakuna tafiti zozote zimefanywa kuhusiana na mielekeo ya wakuu na wahadhiri wa vyuo vikuu.

Hadhi inayopewa lugha katika jamii hutegemea majukumu inayotekeleza katika jamii husika. Lugha inayowasaidia watu katika jamii kwa kutekeleza majukumu mengi yanayowasaidia wanajamii kuboresha maisha yao huchukuliwa kuwa ndiyo lugha bora zaidi na wanajamii

huichukulia kama ya hali ya juu ilhali ile hutekeleza kazi chache na kutoa mchango mdogo au hafifu kwa wanajamii wanaichukulia kamalugha duni na ya kitengo cha chini. Hatimaye lugha hii huishia kudharauliwa na huenda ikapoteza hadhi yake na kubakia kuwa lugha ya wachache tu. Haya ni kwa mujibu wa Sikma(1990). Namna lugha zilivyo na hadhi tofauti ndivyo walivyo wanadamu katika jamii. Nafasi walizonazo katika jamii zinaweza kuheshimiwa na kuchukuliwa kuwa watu bora au wakadharauliwa na kuonwa wa kiwango cha chini. Hadhi ya mtu hulingana na lugha anayoitumia. Kwa sababu hii lugha ya chini iliyodharauliwa hutumiwa na watu wa hadhi ya chini katika jamii. Nao wale wa hadhi ya juu hutumia lugha iliyoheshimika na kuonwa ya hadhi ya juu kwani ndiyo huweza kuwasaidia kuimarisha na kudumisha wakfu wa lugha zao. Hali hii inajitokeza kutokana na hadhi mpya iliyopewa Kiswahilina katiba ya taifa la Kenya ya 2010. Katika hali hii watafiti wa mielekeo ya matumizi ya lugha kama vile Onyango(1990) aligundua kuwa baadhi ya wasomi hata wale wanaotaalamikia Kiswahili huwa hawapendi kukitumia wanapojikuta katika miktadha rasmi bali hupenda kutumia lugha za kigeni kama vile Kiingereza. Baadhi ya watafitiwa aliowachunguza Onyango walidai kuwa Kiswahili hakijakomaa na hakijitoshelezi kimsamiati na kwa hivyo hakipaswi kutumika katika maeneo rasmi. Tutatilia hali hii maanani sana kwa njia za lengo la kutambua iwapo bado mielekeo hii ipo katika kwa wana jamii katika karne hii tukitarajia hali ni tofauti na ilivyokuwa miaka ya tisini wakati Onyango alipokuwa akiufanya utafiti wake ikizingatiwa kwamba lugha hukua kila uchao na inavyokua hadhi inayoambatanishwa nayo hubadilisha mielekeo kwa watumiaji wake. Kiswahilikama kwa sasa kimekomaa na kujulikana hata nje ya taifa kiasi cha kuwa lugha rasmi katika baadhi ya mataifa na kutumiwa kama lugha ya kimataifa.

Ali(2011), alichunguza baadhi ya changamoto zinazowakumba wasemaji wa Kiswahili katika afisi za umma na hata za kibinafsi. Wahojiwa wake walisema kuwa lugha ya Kiswahilini ya kiwango cha chini. Nyakati za kikoloni kulikuwa na mitazamo hasi kuhusiana na Kiswahili. Wabeberu walitumia mbinu zao wakijaribu kukiangamiza Kiswahili ili wapate nafasi za kuendeleza lugha zao za kigeni kama vile Kiingereza Mbatiah M (2012). Hali hii ya mitazamo hasi katika lugha inaweza kuwa ilitokana na mambo kama hayo ya kikoloni. Vilevile hali zingine kama vile umaarufu wa lugha mtu alio nao, asasi za kitaaluma kama vile za kielimu, kijamii, utawala na dini pia zina mchango huo. Haya ni kwa mujibu wa Mathooko (2007:93-98)

Tafiti zinazohusiana na mielekeo ya lugha zilianza miaka ya sitini katika taaluma za saikolojia jamii ambazo zilizofanywa na wataalamu wasomi katika taaluma hizo kama vie Lambert kwa kulingana na Githiora(2008:18).Katika utafiti wake,Lambert aliwachunguza wazungumzaji wa Kiingereza na kifaranza nchini Canada kwa kutumia mbinu ya mlingano fiche.Utafiti wake ulionyesha kuwa waemaji wengi waliotumia lugha hizi mbili walikienzi Kiingereza kuliko kifaranza.Mielekeo iliyosababisha mapendeleo hayo ilisababishwa na masuala ya kihistoria wakidai kwamba Kiingereza kilikuwa lugh iliyowaridhishia wanajamii ufanisi wa kiuchumi.Hali hii si tofauti na hapa nchini Kenya ambapo kutoka wakati wakoloni Kiswahili kilianza kutumiwa kama lugha ya taifa tu huku Kiingereza kikitumiwa kama lugha ya kiufundishaji rasmi.Tafiti za masuala ya mielekeo ya lugha zilianza kufika Afrika miaka ya themanini(1980) na zikaongezeka kufikia miaka ya tisini (1990) Githiora(2008).Hali sasa imekua kwa kiasi ambacho mtu anaweza kuifanyia lugha ya kienyeji utafiti unaohusiana na mielekeo ya watumizi wake.Hii si tofauti na Kiswahilikama lugha ya kienyeji nchini Kenya.

Hisia za lugha hazitoki katika ombwe tupu bali hutokana na baadhi ya mambo ya kihistoria, kidemografia na kijamii. Bourhis katika Ryan na Giles (1982). Katika maelezo yake tunafahamu kuwa sera ya lugha katika taifa ni kiungo bora sana katika ukuzaji na uenezaji wa lugha. Hivyo utafiti huu utachunguza baadhi ya hali zinazoweza kusababisha mielekeo katika Kiswahili na namna hali hizo zinaweza saindia kuleta athari chanya katika Kiswahili kama lugha rasmi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Utafiti wa Mohochi(2011) ambao ulichunguza viongozi na wasomi kuhusu matumizi ya Kiswahilialimaizi kuwa mielekeo huweza kuleta athari kwa watu katika jamii wanapojifunza na kutumia lugha husika.Kwa maoni yake mielekeo hasi au chanya huathiri watu wanapokuwa wakijifunza nankuitumia lugha hasa kutoka wanapokuwa wanafunzi mpaka wanapokomaa na kuwa watu wazima wanapokuwa katika hali ya uamuzi wa kuiteua na kuitumia lugha katika kutekeleza majukumu mbalimbal.Hali hii huenda imewapata wahadhiri na ni jambo la busara kulchunguza swala hili.

Fink (2008) akichunguza mielekeo ya matumizi ya lugha jijini Nairobi, aliwalenga wanafunzi wa chuo kikuu cha Daystar ambao walimpa habari zilizolandana na za Githinji (2008) kwamba watu walikuwa na mielekeo chanya kwa lugha iliyowatambulsha na kinyume chake kwa lugha isiyowatambusha haswa ikilinganishwa na usanifu wa zile lugha zilizohusiana nayo.

Utafiti wa Mukhwana (2008) Mombasa, Nairobi na Kisumu uliochunguza mielekeo ya matumizi ya lugha ulikubaliana na utafiti wa Fink na Githinji. Mukhwana pia aligudua kwamba Kiingereza kilipendwa na wengi hasa katika mazingira rasmi hali ambayo anaeleza kuwa inaweza kuwa inatokana na hali kwamba Kiingereza kinawapelekea kupata ajira nzuri ambayo hubadilisha maisha yao na kuwa bora. Maoni ya Kimemia (2001:120) ni kwamba waKenya wasio wachache huitumia katika shughuli za kijamii na uchumi

Kwa mapitio yale yaliyoandikwa kuhusiana na mada yetu ni kweli kwamba hakuna utafiti wowote uliofanywa unaohusu mielekeo ya wahadhiri wa vyuo vikuu kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa. Kwa hivyo utafiti huu utachunguza mielekeo ya wahadhiri hao wa vyuo vikuu kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa, sababu za mielekeo yao na namna mielekeo hiyo inavyoweza kusaindia kuleta athari chanya katika utekelezaji wa majukumu rasmi kwa Kiswahili.

## **1.8 Misingi ya kinadharia**

### **1.8.1 Nadharia ya makutano na mwachano**

Tutaongozwa na mihimili mikuu na vigezo vya nadharia ya makutano na mwachano iliyoasisiwa na Howard Giles (1982). Ni nadharia ambayo iliendelezwa kutokana na ile ya mawasiliano ya usemi (speech communication theory) ya Leech (1976). Madhumuni ya nadharia hii ya mawasiliano ya usemi yalikuwa kuangazia kwa kina ushikamano ulioo katika jamii na utamaduni wake. Kulingana na Giles, wanajamii ndio wanapaswa kuhifadhi na kudumisha lugha yao kwa kuitumia kutekeleza majukumu fulani kama ya kazi, makundi, mielekeo na hata lugha iliyotofauti na lugha zingine. Hali hii itatusaidia kujua mielekeo ya wakuu na wahadhiri wa vyuo vikuu kuhusiana na Kiswahilina hadhi kilichopewa na katiba ya kutekeleza majukumu kama lugha raami na ya taifa.

Giles aeleza kuwa wanajamii wanapoingiliana hubadilishana ishara, usemi, sauti na mawazo katika miktadha mbali mbali. Hali hii huweza kutokea baina ya makundi fulani au kwa mtu binafsi. Ili mtu aweze kuchukuliwa au ajihisi kama mmoja wa kundi fulani na pengine mshiriki wa kundi hilo, analazimika kujifunza mambo ya msingi ya kundi hilo yanayohusiana na lugha ya kundi hilo. Hii ndiyo hali inayosababisha mafikiano. Kuna aina mbili za ujihusishaji kulingana na mikabala ya nadharia hii ambazo ni ujihusishaji wa makutano na ule wa mwachano (divergence and convergence)

Maelezo ya ujihusishaji kama yanavyoelezwa na msomi huyu katika nadharia hii ni kwamba, wanajamii waishipo karibu na wenzao na wakaanza kuingiliana na kubadilishana lugha na kufikia kitengo cha maingiliano yanayosababisha kundi moja kuacha kuitumia lugha yao na kuhamia ile ya wenzao basi hapo makutano huwa yametokea. Sababu ni kuwa lugha hiyo wameamia wote ndiyo watakuwa wanaitumia kujitambulisha nayo na kuidumisha pamoja na kama kitu kimoja kujitambulisha kwao kunatokea katika mazingira ya kiuchumi, kijamii, kiutawala na kisiasa. Hii ni hali ambayo inaweza wafanya watu wa jamii kuionea lugha hiyo fahari na kuitumia kuendeleza shughuli zao huku wakiichukulia kuwa bora zaidi kwa kwa vile inawasaidia kufanikisha maisha yao kiuchumi na kijamii huku lugha iliyoachwa ikidunishwa na kufifia. Hali hii itatuwezesha kujua ni lugha ipi inayopendelewa kutekeleza majukumu rasmi na wanajamii na visababishi vya hayo mapendeleo ya hiyo lugha katika utekelezaji majukumu rasmi. Visababishi hivyo tutavitumia kutoa mapendeleo na mbinu za kutumia lugha hizi mbili katika miktadha rasmi bila mapendeleo ya lugha moja ili kuzuia kudidimia kwa lugha moja. Katika upande wa ujihusishaji wa mwachano, Giles anaeleza kuwa jamii mbili zikitokea katika maeneo mamoja yanayokaribiana kimaeneo na kwamba kila mojawapo ya jamii hizo iendeleo kutumia, kuhifadhi, kukuza na kudumisha lugha yake kutekeleza shughuli za kila siku za kikazi basi huo ni mwachano. Hii ina maana kuwa kila jamii itaendelea kutumia, kudumisha na kuhifadhi utamaduni wake kwa lugha yake.

Masuala mengine kama vile ya utamaduni, historia, mamlaka, hadhi, mwingiliano wa kutarajiwa, kaida, matumizi ya lugha tarajiwa, utamaduni uliofanana wa jamii hizo mbili na matamaniio ya kibinafsi ni halibambazo husababisha makutano (Turner na Richard (2010)). Hali kama hizi huibua mielekeo iongozayo uteuzi wa lugha fulani kutwkeleza majukumu na hivyo hii itakuwa misingi yetu ya kutambua sababu za kuteua lugha ya Kiingereza au matumizi yake ya kutekeleza majukumu yepi, wapi na kwa njia ipi katika miktadha maalum raami na isiyo raami. Cha kutilia maanani ni kwamba si lazima wanajamii wajihusishe kwa shughuli zao zote kwa wakati mmoja. Wanaweza kujihusisha katika makutano kwa hali fulani na mwachano kwa vitembo vingine. Ujihusishaji wa makutano na wa mwachano huwa yanatokea wakati ambapo jamii mbili zilizo na nguvu tofauti huingiliana katika maeneo fulani na jamii dhaifu ikakubali kutumia lugha ya jamii inayodhaniwa na kuchukuliwa kuwa bora na yenye nguvu zaidi. Watu hufanya hivi kwa manufaa yao ya kiuchumi na kisiasa. Katika hali hii Jamii ambayo inayojihisi dhaifu huanza huiga utamaduni wa jamii inayoonekan kuwa yenye nguvu zaidi na kutumia lugha yake katika

utekelezaji majukumu fulani kujinufaisha katika miktadha ya kiuchumi,kitamaduni kisiasa na kikazi.Hali hii itatupa misingi ya kuchunguza visababishi vya mapendeleo ya kutumia lugha moja hasa kii gereza na kudunisha Kiswahili katika utekelezaji wa majukumu katika mazingira tofauti kama vile kwa nini wanajamii hupendelea kutumia Kiingereza kuandikia barua rasmi kuomba kazi badala ya Kiswahili.Nadharia hii basi itatufaa sana kujua mielekeo ya wakuu na wahadhiri wa chuo kikuu cha Nairobi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa na inavyoathiriwa na Kiingereza katika utekelezaji wa majukumu rasmi chuoni humo.

### **1.9 Mbinu za utafiti**

Sampuli ni hadhira inayotafitiwa na huwakilisha jumuiya nzima. Huchukuliwa kama kundi la utafiti kama wasemavyo Kombo na Tromp (2010). Huwa muhimu katika kupata wahusika wakuwakilisha eneo pana la utafiti (Mugenda na Mugenda (2003).

Katika utafiti wetu tutatumia mbinu ya sampuli kupata data yetu, ambayo baadaye itatumika katika kuchunguza na kufanya hitimisho na mapendekezo.

Tutatumia pia mbinu ya mtabakisho kupata vikundi vidogo vya kuwakilisha eneo zima la utafiti. Vikundi hivi vitakuwa idara za masomo mbali mbali na idara za lugha na mawasiliano katika chuo kikuu cha Nairobi. mbinu hii mtafiti hutabakisha sampuli kwa misingi ya vigezo vinavyomuauni katika mchakato wa uchanganuzi na uwasilishaji wa data.Kwa hivyo vibadala kama vile jinsia zote mili ya kiume,kike na umri wa uongozi na ufundishaji chuoni utatumiwa tukilenga madaktari na maprofesa wanaofundisha chuoni.Sampuli lengwa itatiliwa maanani kama kiwakilishi cha idadi ya wakuu na wahadhiri ambao tutatumia kama sampuli tukijikita kwa maelezo ya Gary (2009) kwamba sampuli lengwa itumike kama kiwakilishi cha jumla ya wanaoshiriki katika utafiti.Hii huweza kuifanya kazi kuwa nyepesi kwa sababu mtu anaweza kukosa wakati na vifaa vya kutuma katika utafiti.Kwa hivyo sampuli lengwa katila utafiti wetu itakuwa ni kiwakilishi cha wakuu na wahadhiri wa vyuo vikuu hapa nchini Kenya utakaofanywa katika chuo kikuu cha Nairobi.

Sampuli inayochukuliwa kama kiwakilishi cha idadi kubwa ya watafitiwa inapaswa kuwa asilimia kumi ya watu wanaofanyiwa utafiti (Mugenda na Mugenda 1999). Utafiti huu basi utatumia asilimia kumi ya wahadhiri wa chuo kikuu cha Nairobi. Japo kwa sasa chuo kikuu kimo katika hali ya marekebicho ambapo ni vigumu kutaja idara ,wahadhiri na wakuu mahususi tutakao watafiti,sampuli ambayo ni ya kimaksudi itatumika kupata data kutoka kwa wakuu na wahadhiri

chuoni katika idara mbalimbali pamoja na za lugha na mawasiliano:Kiingereza,kichina na kikorea.Hii ni kwa sababu hatujui iwapo wote watakubali au watakataa.Tutatumia vibadala kam vile jinsia ya kiume na kike,umri wa ufundishaji chuoni tukilenga madaktari na maprofesa wanaoongoza na wanaofundisha katika chuo hiki kikuu cha Nairobi.

### **1.9.1 Mbinu za ukusanyaji data**

Katika ukusanyaji data, kwa sababu ya maadili yanayokwenda na utafiti, tutajaribu kupata kibali kutoka kwa mamlaka husika. Hata hivyo kwa kuwa utagiti huu ni wa ndani kwa ndani endapo kibali hicho kitacheleweshwa tutafanya utafiti wetu pasi na kibali hicho ila majibu nitakayoyapata hayatatumika kwa sababu nyingine yoyote ile ila kwa sababu za kitaaluma.

Data msingi kutoka nyanjani itakuwa muhimu sana kwani hitakuwa imeshawishiwa kwa njia yoyote na watafiti.Sampuli yetu ya kimaksudi nayo itakuwa muhimu sana katika utafiti huu kwani itatupa wakuu na wahadhiri wenye tajriba kubwa ya utoaji mafunzo chuoni.Wakuu na Wahadhiri hao watakuwa wa msingi sana kwetu kwa matarajio kwamba wana maarifa mengi kuhusiana na jinsi lugha imekuwa ikichukuliwa na kutumiwa na historia ya matumizi yake chuoni.Hali hii itaweza kutupa wanayojua,mitazamo na misimamo yao kuhusu matumizi ya Kiswahilichuoni.

Tutatumia mbinu ya uchunguzi shiriki kwa sababu mimi ni mwanafunzi wa Kiswahili humo chuoni na kwa hivyo nafahamu ni wapi Kiswahili ambapo Kiswahili kinatumika vizuri na ni wapi hakifai kutumika. Nafahamu pia katiba ya Kenya na nafasi ambayo Kiswahilikimepewa.Kwa hivyo mbinu ya uchunguzi shiriki itatumika.

Watafitiwa tunaolenga ni wasomi na watafiti ambao hawana tatizo katika kusoma na kuandika. Kwa hivyo tutatumia hojaji funge na wazi kama mbinu ya kukusanya data. Hojaji kulingana na Kothari (2004) ni maswali yaliyobuniwa na kuandikwa kwa karatasi kwa lengo la kuwauliza watafitiwa ili kupata data za tatizo la utafiti.Kulingana naye anaeleza hojaji kuwa za aina mbili.Hojaji ile funge na ile wazi.Hojaji funge humdhibiti mtu na kumhitaji achague jibu moja kati ya majibu mengi aliyopewa.Hapa mtafitiwa hana uhuru wa kutoa maoni,maelezo au msimamo.Humwitaji mtafitiwa kuchagua jibu moja tu kulingana na namna anavyoelewa maswali hayo.Hojaji wazi nayo humpa mtu uhuru wa kutoa maelezo na maoni kuhusiana na kile anachoulizwa kutegemea mada ya utafiti.Uhuru wa kujieleza husaidia kupata majibu yasiyosawishiwa na watafiti.Kwa hivyo kwa sababu nafahamu kwamba wahadhiri wa vyuo vikuu



pamoja na uongozi wa vyuo vikuu una majukumu mengi huenda nisionane nao ana kwa ana. Kwa hali hiyo mbinu hii ya hojaji itatumika.

Tutatumia uchunzaji kukusanya data kwa kuwatazama wakuu na wahadhiri katika shughuli zao idarani ili tutambue namna wanavyotumia Kiswahili kikilinganishwa na lugha zingine. Katika mbinu hii mtafiti hutazama watafitiwa wakiwa katika shughuli zao za kila siku akithathmini tabia zao kuhusiana na mada inayotafitiwa. Hivyo tutatumia mbinu hii kuangazia kiwango cha umilisi na utendaji wa Kiswahili katika kazi za wakuu na wahadhiri hasa katika utekelezaji wa majukumu rasmi kwa Kiswahili.

Kwa sababu tuna malengo maalum tunayotaka yatimizwe, tutajitokeza na mahojiano ambayo yatalenga maswali yetu ya utafiti na haya mahojiano hayataelekezwa kwa mtu yeyote yule isipokuwa wale walengwa. Pia kuna uwezekano kwamba hao walengwa wasiniambie kila kitu katika hojaji na kwa hivyo kutakuwa na maswali fuatilizwa ambayo yatatokana na hojaji na kwa hivyo ni muhimu kutumia mbinu hizi zote katika utafiti wetu.

Tutatumia hojaji moja yenye muundo maalum kwa sababu maswali ambayo nimetunga ni maswali maalum ambayo yamelenga kupata majibu maalum ambayo yatasaidia kutimisha malengo ya utafiti huo.

Tutatumia kigezo cha likati ambacho kinaorodhesha nambari moja hadi tano:

(i) Nakubali zaidi

(ii) Nakubali

(iii) Nakubali kiasi

(iv) Nakataa

(v) Nakataa zaidi kukubaliana na hoja hiyo.

Kwa hivyo kigezo hiki kitatusaidia kutambua mielekeo hasi na chanya. Hii ni kwa sababu kigezo hiki kimetumiwa na watu wengi akiwemo Mukhwana na kikafaulu.

Tutawahoji wakuu na wahadhiri tubaini wanavyotambua Kiswahili na matumizi ya lugha lugha zingine chuoni. Mahojiano kwa kawaida huwa ni mazungumzo kati ya watu wawili, watatu au zaidi

kuhusiana na mada fulani(Kothari 2004).Mtafitiwa katika mahojiano huulizwa maswali na mtafiti huku naye akiyajibu.Tutatumia mbinu hii kwa lengo la kutambua mitazamo ya watafitiwa tunaolenga kuwatafiti kuhusu Kiswahili na jinsi wanavyokichukulia kama kama lugha ya kutekeleza wajibu rasmi.Maswali yatalenga mitazamo na mielekeo ya matumzi ya lugha mbali mbali chuoni.

Majibu tutakayoyapata tutayahifadhi katika kanda za kunasa sauti na simu rukono.Pia kwa sababu ya msambao wa janga la virusi vya korona ambalo linazuia watu kutangamana moja kwa moja baadhi ya mahojiano yatafanywa kwa njia ya simu au ya mtandao kwa wahadhiri ambao wanaweza kutupa habari na ambao ni vigumu kuwafikia.Baadhi ya watafitiwa tutawahoji moja kwa moja.Tutawahoji wanafunzi huko chuoni pale ambapo itabidi.Lakini kwa sababu ya mipaka yetu ya utafiti wetu wanafunzi hawahusiki.Hata hivyo dhana ya wanafunzi ina mapana na marefu yake kwa sababu hata mwanafunzi aliye na shahda ya uzamifu hujiona kwamba bado anajifunza na kwa hivyo ikitokea mtu amejiiita mwanafunzi basi atakuwa amejumuishwa katika utafiti wetu.

Majibu yao yatatupa data ya kuaminika. Lugha zitakazotumiwa katika mahojiano hasa katika kuandika maswali ya hojaji ni Kiswahili na Kiingereza.Vile vile tutaitumia mbinu ya uchunguzi kupata habari halisi kutoka kwa watafitiwa hususan wakuu wa chuo.

### **1.9.2 Mbinu za uchanganuzi wa data**

Kabla ya kuchnganua data yetu tutaiweka katika makundi yanayolandana huku tukijifunga kwa vipengele vya mielekeo na mitazamo inayotawala matumizi ya lugha.Tutatambua lugha inayotumiwa katika miktadha maalum kwa kumakinika katika kuchambua video tutakazonasa kutoka kwa watafitiwa,majibu ya hojaji na majibu yatakayobainika kutokana na mahojiano.Mazungumzo tutakayonasa kutokana na watafitiwa yatatusaidia kutambua mieleko na mitazamo ya matumizi ya Kiswahili kikilinganishwa na lugha zingine kama vile Kiingereza ambacho hutekeleza majukumu rasmi katika maeneo sawa na lugha ya Kiswahili.Hali hii itatuani kutambua ni miktadha ipi lugha Kiswahili hutumiwa na ni ipi Kiingereza na lugha zingine hupendelewa na sababu za mapendeleo hayo.

### **1.9.3 Uwasilishaji wa data**

Matokeo ya ufasiri wa data yatakayoibuka kutokana na uchanganuzi wa data tutakayoichanganua,tutayadhihirisha kwa njia ya vielelezo kama vile vya miraba ya kuchora, michoro ya paichati na michoro ya kimviringo itakayoonesha asilimia ya matumizi ya lugha fulani

na hata grafu.Kwa kufanya hivi tutaonyesha kwa michoro ya kimviringo ni asilimia ngapi ya watumiaji wa lugha hutumia lugha ipi na katika miktdha gani.Tutaonesha idadi ya wakuu na wahadhiri:Madaktari na maprofesa tutakaowatafiti huku tukidhihirisha lugha wanazopendelea kuzitumia kutegemea muktadha.Kwa kufanya hivi tutawarahisishia wale wasomji wa kazi hii kutafsiri matokeo ya utafiti.

## **SURA YA PILI**

### **2.0 HISTORIA YA MIELEKEO YA KISWAHILI NCHINI KENYA**

#### **2.1 Utangulizi**

Mielekeo ya wakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi itaeleweka vyema na kutufahamisha misimamo yao kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa kutokana na mapitio ya Kihistoria ya mielekeo ya lugha hasa ya Kiswahili Kenya. Mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili huzuka na kubadilika kila uchao kutokana na hali kwamba Kiswahili hukua kila uchao na watumiaji wake huweza kuibua mielekeo wanapokitumia kutegemea faida na hasara zinazojiri. Mapitio ya historia ya mielekeo ya Kiswahili kupitia vipindi mbalimbali vya ukuaji na maendeleo ya Kiswahili yatatusaidia kuelewa mielekeo na misimamo ya wakuu na wahadhiri wa chuo kikuu cha Nairobi. Kwa mujibu wa Kembo Sure (2009), ili kufahamu mielekeo ya lugha miongoni mwa washikadau wa utekelezaji wa masuala ya sera ya lugha, ni jambo la busara kuipitia mielekeo ya wakenya kabla ya majio ya Mkoloni, enzi ya Mkoloni na hata baaada ya kuunyakua uhuru. Hii itatusaidia kujua mielekeo ya Kiswahili katika vipindi mbalimbali vilivyosababisha ueneaji wa Kiswahili pwani na barani Afrika. Maingiliano ya watu, maendeleo ya Kibiashara, za Kidini, Kikoloni na uharakati wa uhuru tumeyashughulikia kama baadhi ya visababishi vya ueneaji wa Kiswahili Whiteley (1969). Hivyo, historia hii ya mielekeo ya Kiswahili itakuwa muhimu sana katika utafiti wetu.

#### **2.2 Kipindi cha ukoloni**

Waafrika waligawanywa na wakoloni katika mataifa mbalimbali walipokongamana mjini Berlin Disemba 1884 hadi 1885 ili kuangazia matukio na matumizi ya Kiswahili katika kipindi hiki tutakiangalia katika awamu tatu. Kwanza, kabla ya vita kuu ya pili ya dunia, kuanza wakati wa vita kuu ya pili na baada ya vita kuu ya pili.

Mielekeo katika kipindi hiki cha ukoloni, kimegawanywa kutatu ambako tumeshughulikia kipindi kabla ya vita kuu ya kwanza ya dunia, baada ya vita kuu ya dunia hadi vita kuu ya pili ya dunia na tatu kabla ya uhuru wa Kenya.

##### **2.2.1 Kabla ya vita kuu ya pili ya dunia**

Wakati huu wa kipindi hiki, washikadau wengi waliunda sera mbalimbali za lugha. Baadhi ya washikadau hawa ni wamishenari. Nabea (2009). Lengo kuu la wamishenari lilikuwa kueneza injili

ya Kikristo. Nia na maamuzi ya mateuzi ya lugha ya kueneza injili ilitofautiana miongoni mwa wamishenari. Tofauti za mapendeleo ya maamuzi ya lugha ya kueneza injili yaliibua mielekeo tofauti ya matumizi ya Kiswahili kati yao.

Baadhi ya wamishenari walipendelea kueneza injili kwa Kiswahili kwakuwa kilikuwa lugha sambazi nyakati hizo. Hata hivyo wamishenari wa baadaye walikipinga wakidai kwamba kilihusishwa na kiarabu kueneza dini ya kiislamu. Walikionakama lahaja ya kiarabu Mbaabu kutokana na mafungamano ya lugha hii na maenezi ya dini ya Kiislamu Mbaabu (1991:8).

Wamishenari waliopendelea matumizi ya lugha ya kiasili nchini Kenya walikuwa na mielekeo hasi kuhusu Kiswahili. Vilevile, wakoloni walipendelea kuwafundisha waafrika Kiingereza ili wapate watumishi katika afisi zao na watumwa wa kiakili na wa kiitikadi. Huu ni mwelekeo hasi wa Kiswahili uliodhihirishwa na wakoloni kwa kuwa Waafrika wengi walifanya bidii kufanya Kiingereza ili wapate ajira na vilevile waweze kujinasibisha na wakoloni wa Kiingereza.

Kufikia 1901, kongamano la wamishenari wa *United Missionaries to Central Africa* lililoandaliwa lilijadili masuala ya lugha na elimu kuagiza kwamba lugha za kiasili zitumiwe kufundishia viwango vya chini vya elimu ya shule ya msingi kuanzia darasa la kwanza mpaka la tatu na Kiswahili kufundishwa darasa la nne na la tano kisha madarasa yaliyobakia yafundishwe kwa Kiingereza mpaka chuo kikuu. Hali hii ilidhihirisha kwamba mielekeo ya Wamisheni katika elimu kuhusu Kiswahili ilikuwa isiyokipinga na isiyokikubali. Hii ndio sababu waliamua kwamba kitumike kufundishia madarasa ya katikati na wala sio ya mwanzo au ya mwisho katika mfumo wa elimu Kenya.

Kufikia 1919, tume ya elimu ya kikoloni iliunga mkono ufundishaji wa Kiswahili na kusisitiza kwamba Kiswahili kifundishwe kikiwa somo la lazima. Somo la Kiswahili lilikuwa linashushwa hadhi na kupandisha hadhi ya Kiingereza na lugha za kiasili kutegemea matakwa na matarajio yao wakati huo. Kutokana na matarajio yao, mkurugenzi wa elimu aliyekuwepo wakati huo J. Rorr alionyesha mwelekeo hasi wa Kiswahilina kupinga ufundishwaji wa Kiswahili kama somo la lazima akidai kwamba ni kupoteza wakati.

Kulingana na maelezo ya Mbaabu (2007), Tume ya Phelps Stokes ilipozuru Kenya 1924, kuliibuka malalamishi kutokana na mzozo uliokuwepo kati ya wakoloni, walowezi na wamishenari. Kutokana na hali hii, tume hiyo ilipendekeza lugha ya kiasili zitumiwe kufundishia

wanafunzi shuleni. Kiswahili kitumiwe katika maeneo ilikokuwa lugha ya kwanza kama pwani na Kiingereza kitumiwe katika ngazi za juu kama shule za upili na chuo kikuu. Hii ni baada ya tume hiyo kugundua kwamba wafrika ambao walikuwa wazazi wangepeleka watoto wao shuleni iwapo shule hizo zingetumia kiswahili. Kufundishwa kwa Kiswahili kulikuwa kama kichocheo cha wazazi wafrika kupeleka watoto wao shuleni.

Ijapokuwa Kiswahili kilikuwa kichocheo cha wazazi kuwapeleka wanao shuleni na kwamba kilikuwa lugha sambazi wakati huo, wakoloni, walowezi na wamishenari hawakuwa na mielekeo chanya kwa Kiswahili kikilinganishwa na za kiasili ambazo zingewasaidia kuwagawanya Wakenya kwa misingi ya kikabila na kuwatawala kirahisi. Hata hivyo mnamo mwaka 1925, mkutano wa usanifishaji wa Kiswahili uliandaliwa Dares salaam kwa lengo kwa kuteua lahaja moja isanifishwe kwa lugha sanifu, lahaja ya Kiunguja iliteuliwa na kusanifishwa. Hatua hii uliimarisha Kiswahili na kuweza kuwa lugha ya Kiswahili sanifu iliyokubaliwa kote katika mataifa ya Afrika Mashariki. Hiini idhibati kwamba katika kipindi hiki na kwa hatua hii mielekeo ya wakoloni watawala na wamisheni kuhusu kiswahili ilikuwa chanya kwa kuwa walitaka kukikua na kukiimarisha katika misingi ya lugha za ulimwenguni hapa zilizosanifishwa. Kutokana na hatua hii vitabu na kamusi za hapo awali ziliweza kurekebisha ili ziendane na hiki kiswahili kipya kilicho sanifu. Katika kufanya hivi hela zilitumika pamoja na rasilimali watu na hii ni idhibati nyingine ya kuonyesha kwamba mielekeo ya wakoloni watawala kuhusu Kiswahili ilikuwa chanya. Hii ni kukiendeleza Kiswahili sanifu kimaandishi. Wandishi wa kazi bunilizi walitiwa motisha ya kuandika kazi zilizochapishwa kwa kiswahili na kampuni ya East African Literature Bureau. Juhudi hizi za kukichangamkia Kiswahili ndizo zilizozalisha waandishi kama vile Katalambula na Shaaban Robert ambaye anatajwa kama baba wa fasihi leo ya Kiswahili. Hapa kinachodhihirika ni mwelekeo chanya kuhusu Kiswahili enzi ya Ukoloni wa mwingereza Kenya kabla ya vita kuu ya pili ya dunia.

### **2.2.2 Wakati wa vita kuu ya pili ya dunia**

Kipindi hiki kilianza 1939 hadi 1944. Katika kipindi hiki si mambo mengi yaliyotokea kuhusiana na lugha kwani ni kipindi kilichohanikiza ukosefu wa usalama, hivyo wengi walirudi makwao kupigana. Baadhi ya Waingereza walirudi kwao kupigana vita vilivyokuwa vikiendelea. ukosefu wa usalama ulionyesha hatari kubwa iliyosababisha sera zilizopendekezwa za lugha kuwa na athari

chanya na zingine hasi katika lugha ya Kiswahili kwa Wakenya. Jambo la kimsingi katika kipindi hiki kama kulivyokuwa wakati wa kile cha vita kuu ya kwanza ya kidunia ni kwamba Wakenya walishiriki vita hii. Mafunzo yao ya kivita yalitolewa kwa lugha ya kiswahili kwa sababu ndiyo ilikuwa lugha unganishi. Wakenya hawa walitumia lugha hiyo kuwasiliana vitani na kijamii. Hapo kulijengwa mwelekeo wa ushikamano na ushirikiano miongoni mwao. Waliporudi Kenya baada ya vita walipewa makazi katika mitaa ya Kiswahili kama vile ya Kariakoo mjini Nairobi na ambayo haikujua ukabila. Kutokana na hali hii mielekeo kuhusu Kiswahili ilijidhihirisha kama ya undugu, upendo na ushirikiano. Istoshe wanajeshi hawa wa Kikenya waliporudi vijijini kwao walikozaliwa waliweza kuigwa kama mashujaa waliopigana vita ya kwanza na ya pili ya dunia ya dunia na wakarudi salama baada ya kuunganishwa na Kiswahili. Hali hii vile vile ilijenga mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili. Kamati ya mashauri kwa mkoloni ilitengenezwa 1941 kutafuta njia mwafaka za kuwafunza Wafrika kusoma na kuandika (Mbaabu 2007). Kuundwa kwa kamati hii kilipendekeza masuala yaliyoibua athari hasi katika kiswahili kwa kuwa ilipendelea kisomeshwe kwa lugha za kiasili na Kiingereza. Katika kipindi hiki cha vita kuu ya kwanza ya dunia Tume ya Beecher (1942 hadi 1948), iliundwa kwa lengo la kushughulikia ufundishwaji wa lugha katika shule za Kiafrika. Ripoti yao ilipendekeza kutumiwa kwa lugha za kiasili na nafasi ya Kiswahili ichukuliwe na Kiingereza kutekeleza majukumu ya kimawasiliano Kenya. Ripoti hiyo ilikipinga Kiswahili kutumika kuendesha shughuli za Kielimu hasa 1943 ambapo katika kumbukumbu za ofisi ya mkoloni walipotilia mkazo kutumia lugha za kiasili na Kiingereza katika shule za waafrika. Kupingwa kwa Kiswahilina na mapendekezo ya tume hii kulitokana na hali kwamba, kiswahili kilionekana kuwa kimeomba misamiati kutoka kwa lugha ya kiarabu Mazrui (1978:228). Kwa mujibu wa Gorman (1974:405) madarasa yalijengwa na wamishenari ili kufundishwa kwa somo la Kiingereza kama somo la lazima na Kiswahili kutumiwa kufundishia masomo mengine na lugha za kiasili kufunzia madarasa ya kwanza, Kiswahili kikifuata Mbaabu (1996:5-6). Hali hiyo iliwafanya wafrika wasifunze Kiingereza kwa kuwa kundiyo lugha ilionekana kuwa na manufaa kwao kuwapa ajira ya kazi bora na kuacha kujifunza Kiswahilina kuiona lugha isiyo na manufaa yoyote. Huu ulijitokeza kama mwelekeo usio kubalifu kuhusu kiswahili.

### **2.2.3 Baada ya vita kuu ya pili ya dunia**

Kufikia mwisho wa vita hii ya pili ya dunia 1948, Kiswahili klitumiwa kusomeshea vitengo vya chini katika shule za sekondari na kusomeshwa kutoka darasa la tatu na kuendelea.

Ripoti ya pili ya Tume ya Beecher ilitoa ufafanuzi wa mapendekezo yaliyofanywa na tume hiyo 1942 kwamba lugha za kienyeji ishirini zitumiwe shule za msingi zikiwemo Kikuyu, Kimeru, Kikamba, Kidawida, Kimaasai, Kisomali, Kigirama, Kipokomo, Kijaluo, Kigala, Kikisii, Kiborana, Kiteso, Kitaveta, Kitende, Kisule na Kiturkana.

Ili kuzikuza na kuimarisha lugha hizo, shirika la Kuchapish vitabu *la East Africa Literature Bureau* 1950, likaagizwa kuchapisha vitabu kwa lugha ishirini za kiasili. Hata hivyo, kwa ukosefu wa rasilimali na wingi wa vitabu shirika hilo halikuweza kuchapisha vitabu kwa lugha hizo za kienyeji zote. Kwa mujibu wa Mbaabu (2007), ijapokuwa Kiswahili kilididimishwa na kukuzwa kwa lugha za kiasili, vitabu vya Kiswahili viliweza kuchapishwa na shirika hilo.

Kwa mujibu wa Mazrui na Mazrui (1995) katika kipindi cha miaka ya hamsini (1950) Kiswahili kilipigwa marufuku katika sekta za serikali na elimu. Wakoloni walipinga Kiswahili kwa hali zote ili kuhahakisha kuwa waafrika hawana umoja wa lugha ya kuwasiliana ili wasiwe na umoja wa kupigania uhuru wao. Hali hii ilizua vuguvugu la Mau Mau ili kupigania uhuru wao na kusababisha kutangazwa kwa hatari nchini Kenya 1952. Wakati huo wakoloni waliendeleza Kiingereza kwa waafrika ili kuendeleza utawala wao hata baada ya Waafrika kupata uhuru.

Mwaka huo wa 1952, kitabu cha *Africa Education* ambacho kilisisitiza kukomeshwa kwa haraka kusomeshwa kwa Kiswahili kikidai kuwa Kiswahili kilikuwa jabali kubwa katika maendeleo ya Kiingereza. Kutokana na maelezo ya kitabu hiki, Kiingereza kilikuwa ni lugha ya kipekee ya maendeleo ya kiufundi, elimu na kisiasa. Kitabu hicho kilieleza kuwa Kiingereza ndiyo lugha ambayo ingeunganisha Wakenya zaidi kuliko Kiswahili na zaidi ya hayo Kiingereza kilikuwa lugha ya kimataifa. Hali hii inaonyesha mwelekeo hasi kuhusu Kiswahili.

Tume ya *The East Africa Royal Commission* ilibuniwa 1953 ambapo iliidhinisha Kiingereza kitumiwe kusomeshwa madarasa ya chini na kitumiwe kusomesha madarasa mengine wanafunzi wanapoanza kukielewa. Mikakati iliyokuwa imebuniwa ya kufundishia Kiswahili ilitupiliwa mbali 1957 ambapo katika shule za Aga Khan madarasa 30 ya kwanza yalitumia Kiingereza katika shule za elimu kama lugha ya kufundishia darasa la kwanza. Mfumo huu ulibuniwa 1961. Ulipowadia 1962, shule mjini Nairobi zilikuwa zimeanza kutumia Kiingereza kufundishia darasa la kwanza.

Mtihani wa *Kenya Africa Preliminary Examination* uliofanywa 1961 ambao ulilenga kuwachuja wanafunzi kuingilia sekondari ulitupiliwa mbali na pengo hilo likazibwa na mtihani wa *Kenya*



*Primary Examination.* Katika mtihani huu, Kiswahili kiliondolewa kabisa na hakikutahiniwa katika mtihani huo.

Kulingana na Chieni(2001),shule za Waafrika zilikuwa chache.Kiingereza kilifundishwa kama somo bali si ja lugha ya kufundishia.Wafrika waliohitimu na kufuzu kutokana na hizo shule walikuwa wameijenga misingi dhabiti ya hoyo lugha.Waafrika hao walichukuliwa kama wasomi katika jamii.Sera hiyo ya lugha ilileta utabaka wa kielimu mpaka waafrika wengi wakatamani kujifunza lugha hiyo.Waliofuzu katika shule za wakoloni na waliofahamu kiingereza walipata ajira katika ofisi za wakoloni.Sera hii ilikuza Kiingereza na kukitinga Kiswahili kama asemavyo Mukhwana (2008) . Mielekeo hii iliathiri Kiswahili kwa muda mrefu hata baaday ya uhuru ambapo wakenya wengi waliamini kuwa ili mtu apate ajira bora lazima ajue kuongea Kiingereza.Hii inaashiria kuwa wakoloni na wamishenari walikipinga Kiswahilina kupendelea Kiingereza na lugha za kiasili wakidai kuwa lugha ya Kiswahili ilikuwa kizingiti katika maendeleo ya taifa.

Kulingana Chiraghdin na Mnyampala, kuna sababu kadha zinazosababisha kuwepo kwa mielekeo hasi ya Kiswahili na Wakenya ikiwemo:

- i. Kiingereza kiilihusishwa na watu wa tabaka la juu la wasomi na watawala ambao walionewa fahari kuliko wasiokijua Kiingereza
- ii. Kiingereza kilihusishwa na daraja la ajira bora, vyeo muhimu vya kisiasa, kibiashara, kielimu na kiuchumi ambavyo vilisaidia wakenya kujiendeleza kiuchumi.
- iii. Wakenya walishapotoshwa na Mkoloni kuwa lugha asili ni za watu wasiostaarabika na kwa hivyo hawakuona haja kujifunza lugha zao
- iv. Usanifishaji wa Kiswahili kama lugha ya kiasili ulifanywa na wakoloni wenye asili ya Kiingereza na kijerumani. Hali hii ilileta utata miongoni mwa wakenya ikaonekana kama ngumu kuisoma kutokana na sababu tofauti za kiothografia, za kisarufi na za kimatamshi.
- v. Walimu na wakuu shuleni waliwapa adhabu wanafuu waliozungumza kwa lugha zao za kiasili shuleni na kufedheheshwa kwa kubebeshwa mabango yenye maandishi yaliyosoma "Mimi ni mjinga sijui Kiingereza"(I am a fool i don't know English) Wathiong'o (1986:11).Ili kuepukana na fedheha za aina hii,wakenya waliacha kutumia lugha zao na kuibua mielekeo hasi kwa lugha zao.Hatua hizi zilizochukuliwa na wakoloni wa Kiingereza na wakuu wa Kiafrika ziliangamiza Kiswahili na kusababisha mielekeo hasi

kwa lugha ya kiswahili wakati huo.Ni wakati huu mielekeo hasi kuhusu kiswahili ilionekana wazi kwa wafrika waliokuwa wakitumia Kiswahili.

#### **2.2.4 Baada ya Ukoloni**

Katika kipindi hiki, Kenya ilikuwa imepata uhuru 1964.Kiingereza bado kilikuwa kinachukuliwa kuwa lugha bora zaidi kuliko Kiswahili kutokana na mashiko yaliyowekewa lugha hiyo katika kipindi cha ukoloni. Kiingereza kilionekana katika mashirika mbalimbali kupewa hadhi ya juu kuliko Kiswahili (Chieni 2001).

Makabila ambayo hayakuwa ya kibantu kama vile kabila la kijaluo yalikibagua Kiswahili wakidhani lugha hiyo ingewabagua kimaendeleo (Chimerrah 1998). Kulingana na Chimerrah kilikuwa kinaya wao kusema kulikuwa rahisi kwao kujifunza Kiingereza kuliko Kiswahili.Baadhi ya wasomi na viongozi hawakuwa tayari kujifunza Kiingereza kikamilifu wala kukijengea misingi madhabuti.Walipendelea kutumia Kiingereza walipotaka kuongea mambo rasmi katika mianda rasmi badala ya kiswahili.Kulingana na Chimmerrah ,Kiswahili kilitumiwa pindi tu walipotaka kusoma mambo ya undugu miongoni mwao na walipozungumzia masuala yasiyokuwa rasmi.Kwa vile walikuwa wasomi wa Kiingereza walifanya hivyo ili kujitenga na jamii pana kuonekana kama wasomi.

Misingi ya uundaji wa sera ya lugha ilikuwa katika karne ya kumi na tisa.Wakati wa kipindi cha ukoloni wanamishenari walishindwa kutumia lugha za kiasili kueneza injili ya kikristo.Mwaka wa 1901 wamishenari walikongamana katika kongamano la (United Missionary Conference) walishindwa kutumia lugha za kienyeji kuwasiliana.Lugha iliyoonekana murua wakati huo ilikuwa ni Kiswahili Muthiani(1986).Kutokana na hali hii wanamishenari ambao ni Askofu Steer,Ludwig Krapf na John Rebman walianza kufanya utafiti wa lugha hatua moja baada ya nyingine. Mbaabu(1991:8).Walianzisha asasi zilizokuwa za kimishenari kama vituo vya kimishenari vya kuendesha biashara,elimu na matibabu Mukhwana (2008).Misamiati ya Kiswahili ilifunzwa katika asasi hizo.Msukumo wa ufunzaji Kiswahili ulitiliwa maanani katika asasi hizo na kupelekea vitabu vya Kiswahili kuchapishwa.Kulingana na Chiraghdin na Mnyampala (1977:54),Chini ya uongozi wake Dkt.J.L Krapf na kasisi Steer,waliendeleza Kiswahili kwa kuandika vitabu vya Kiswahili vya sarufi,kutunga kamusi kwa lugha ya Kiswahili na vitabu vingine vya kufundishia injili kwa Kiswahili.Mbaabu (1991:9-19) anasema kwamba,wamishenari walishindwa kuteua lugha ya kutumia kusanifisha kiswahili.Kwa vile sajilii iliyokuwa ikitumika

ni ya dini ya kikristo,waarabu waliokuwa wakitumia Kiswahili wakaibua mielekeo hasi kuhusiana na Kiswahili.Mielekeo hii ndiyo inayoonekana mpaka leo.

Wakati huo wakoloni hawakuwa na sera ya lugha mahususi ya kutumia.Hivyo C.Hobley aliyekuwa mkuu katika mkoa wa pwani wakaa huo alipendekeza Kiswahili na Kiingereza zisomeshwe Gorman (1974:406).Hata hivyo waliichukulia kwamba lugha iliyokuwa na uwezo wa kuongoza utamaduni bora kuliko lugha zingine zote za kiasili ni Kiingereza Jones(1925:8).Wakoloni walitumia mbinu zote katika sera ya lugha kuwatenganisha wafrika kwa kupanua mipaka ya lugha ili waweze kuwatawala Gorman (1974:426).Hapa ndipo lugha ya Kiingereza ilikuwa na kupewa hadhi ya juu na lugha za kiafrika zikadunishwa na kuchukuliwa za hadhi ya chini.

Katika kipindi hiki cha baada ya ukoloni, mielekeo inayohusu Kiswahili tumejadili tukizingatia namna lugha hii ilivyotumiwa katika sekta ya elimu, uwanja wa kisiasa na kuendeleza shughuli za umma katika vyombo vya habari tukilenga kubaini mielekeo inayohusu Kiswahili na nafasi yake katika matumizi yake sasa.

Baada ya kuupata uhuru, tume mbalimbali ziliweka mikakati ya namna lugha zingetumiwa. Tume ya elimu ilifanya utafiti 1964 ili kubaini maoni ya wakenya kuhusu matumizi ya lugha. Matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa wakenya walipendelea kutumia lugha za kiasili katika mawasiliano ya kawaida ya kijijini kwa mdomo nacho Kiswahili na Kiingereza zitumiwe katika masomo kutoka shule za msingi mpaka vyuoni. Kiswahili kilikuwa nguzo ya umoja na kuunganisha wakenya. Kando na umuhimu huo, kilipuziliwa bila kutiliwa mkazo katika mitaala ya elimu.

Wakati huo tume ya Ominde ilitoa ripoti iliyoonyesha kuwa wakenya walionyesha ukubalifu wao wa kutumia Kiingereza katika sekta ya elimu mpaka chuo kikuu. Tume hii ilikikua Kiingereza kuliko lugha zingine ambazo ni Kiswahilina na lugha za kienyeji. Kiswahili na lugha za kienyeji zilipendekezwa kutumiwa katika sekta mbalimbali za elimu. Wakati huo, taasisi ya elimu ilianza kuchapisha vitabu kwa lugha za kiasili Kiswahili kikiwepo na Kiswahili kikaanza kutumiwa kufundishia masomo ya gumbaru (1967).

Utafiti wa sera ya lugha uliendelea kufanywa na tume ya Wamalwa 1971 na ikabainika kwamba ,wengi wa wafanyakazi walikuwa waafrika na hivyo walikuwa na uwezo wa kuwasiliana

kwa urahisi kwa kiswahili. Ukweli ulibainisha kwamba, kulikuwa na wafanyakazi wengi wa Afrika ambao hawakukijua kiswahili. Hivyo kukatolewa mapendekezo kuwa kozi za Kiswahili izianzishwe katika taasisi za utawala, vyuoni na katika taasisi za serikali ambapo zilianzishwa kabete na maseno kwa mujibu wa Mbaabu (1996), taasisi hizo zilianza kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa umma kwa kiswahili.

Kufikia 1976, tume ya Gachathi ilikikiza Kiingereza na kukipa hadhi ya juu zaidi. Ilipendekeza kiingera kutumiwa kufunzia darasa la nne mpaka chuoni japo ilionyesha Kiswahili kama lugha muhimu, Kiswahili kilikuwa kikionekana kama cha hadhi ya chini katika mitaala ya huko shuleni. Katika ratiba ya ufundishaji shuleni, Kiingereza kilipewa masaa mengi ya kufundishia ilhali Kiswahili kilipewa masaa tatu tu. Hali kadhalika, Kiswahili hakikutahiniwa katika mtihamu kinyume na kilivyokuwa Kiingereza kilichotahiniwa na kuwasaidia wakenya kupata kazi. Hali hii iliwafanya watu kutilia maanani na kumakinikia kwa Kiingereza kuliko Kiswahili

Tume ya Mackey ilipoteuliwa 1981, ilipendekeza mfumo uliokuwa mpya wa elimu 8.4.4 badala ya ule uliokuwepo wa 7.4.3.2. Tume hii ilipendekeza Kiswahili kuwa somo la lazima na litahiniwe shule za msingi na ngazi za juu za vyuo vikuu. Kiingereza kilitakiwa kiwe lugha ya kufundishia.

Pendekezo hili la Mackey lilipelekea watu wengi kumakinika kwa Kiswahili na idara ya Kiswahili ilianzishwa Chuo Kikuu cha Moi 1987. Hali hii iliendelea katika vyuo vingine kufundisha Kiswahili kama kozi ya lazima katika idara za mawasiliano.

Tume hii ilikiuza Kiswahili na kukionea fahari baada ya kupendekeza vitabu vya Kiswahili vichapishwe ili wanafunzi wapate vya kusoma na walimu wapate vya kufundishia.

Mpango wa maendeleo ya kitaifa wa 1984-1988 ambao ulichapishwa 1983, Kiswahili kiwekwe katika kategoria moja na lugha za kienyeji ili kitumike kufundishia somo la gumbaru. Wanafunzi nao wakalazimishwa kuwafiliana kwa Kiingereza kwa kuwa masomo yalitahiniwa kwa Kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili.

Mbaabu (1996), anaeleza kuwa wanafunzi waliofanya mtihamu wa kwanza hapa nchini baada ya pendekezo la Mackey la kutahiniwa kwa Kiswahili 1989, wengi wao walisemekana kufanya vizuri katika mtihamu wa Kiswahili kuliko vyuo vikuu vilivyokuwepo wakati huo. Hizi zilikuwa kauli ya waziri wa elimu wakati huo 1989, Peter Oloo.

Bodi iliyosimamia mitihani wakati huo, ilipendekeza wanafunzi wawe na alama ya C+ na zaidi ili waweze kujiunga na vyuo vikuu. Kati ya wale waliokuwa na ari ya kufanya Shahada katika sanaa, elimu na ufundi walihitajika wawe wamepata somo la Kiswahili. Ni wakati huo vyuo vya utoaji wa masomo ya ualimu vilipaswa kufunza kiswahili. Mpango wa Kimaendeleo 1979-1983 uliochapishwa ulihitaji kuanzish taasisi ya Kiswahili humu Chuo Kikuu cha Nairobi. Ulisema “chuo kitaanzisha mtaala Kiswahili ili kusaidia kutoa maandishi ya kutosha na makala nyingine ya elimu ya ufundishia wa Kiswahili shuleni. Uchunguzi ulifanywa wa uwezekano wa kuanzisha taasisi ya uchunguzi wa Kiswahilichini ya mpango huu” (mpango wa maendeleo, 1979-83:166).”

Kiswahili kilifundishwa vyuoni kama kozi. Chuo Kikuu cha Nairobi kilianzisha idara ya isimu na lugha za kiasia 1969. Kufikia 1978- 1985, chuo kikuu cha Kenyatta kikaanzishwa kama chuo kishirikishi cha chuo kikuu cha Nairobi kama chuo cha ualimu kilichofundisha shahada ya kwanza, uzamili na uzamifu katika Kiswahili. Vyuo vingine baadaye vilivyochipuka na vilivyofunza Kiswahilikama kozi katika shahada ya kwanza ni chuo kikuu cha Egerton na Maseno. Hali hii ilionekana mpaka sasa katika vyuo vya umma ambapo mabewa yake yanafunza Kiswahilikatika vyuo vya elimu. Vyuo vingine hata vya kibinafsi vikaweza kufundisha Kiswahilikatika shahada ya kwanza, uzamili na uzamifu. Kwa mfano: Methodist, Nazarene, Baraton, Mount Kenya, Catholic, Kabarak, St. Paul na vingine vingi. Hii inaonyesha kuwa Kiswahili kimepokelewa kwa njia chanya kuliko kipindi kilichotangulia cha ukoloni.

### **2.2.5 Sekta ya elimu**

Kenya ilipopata uhuru 1963, watu wengi walikuwa wamejifunza kiswahili. Hali ya matumizi ya Kiswahili ilidhihirika katika kampeni za kisiasa. Mwaka wa 1969, mswada ulipitishwa bungeni kuwa Kiswahili kiwe lugha rasmi. Mswada huo ulipata washiriki waliounga mkono na wengine kuupinga. Aliyekuwa mwanasheria mkuu Charles Njonjo aliupinga kwa kudai kuwa Kiswahili ilikuwa lugha ya kiarabu na hivyo ilikuwa lugha ya kigeni kilivyo Kiingereza. Kariuki G. G aliongezea kuwa kilikuwa lugha ya waislamu ya kuendeshea shughuli zao za kidini. Wengine walidai kuwa, Kiswahili hakikuwa kimekomaa na hivyo kilikosa mizizi na ukomavu wa misamiati ya kutosha ya kisayansi na kiufundi. Kwa hivyo, kwa maoni yao ujifunzaji wa Kiswahili ulikuwa kupoteza pesa na wakati na kwamba kingewatenganisha wale lugha zao za kwanza hazikuwa Kiswahili na kuwapa kazi za mishahara midogo. Mielekeo hii hasi ilitokana na wakoloni wakati wa ukoloni.

Kulingana na Mbaabu (1996), chama cha utawala *Kenya African National United (KANU)* 1970, waliibua mikakati ya kukifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi.

Mzee Jomo Kenyatta ulipendekeza mswada huo pia na kuupitisha. Mzee Jomo Kenyatta alipenda kuitumia Kiswahili katika hotuba kuhutubia wakenya. Kiswahili kilipata hadhi ya juu kuliko hapo awali. Aliyekuwa Katibu mkuu mtendaji wakati huo Robert Matano, alitangaza mipango hiyo 1974 kwa serikali ilikuwa itekeleze mpango huo kwa awamu mbili:

Awamu ya kwanza itekelezwe 1971 ikiwahitaji Wakenya wakizungumze Kiswahili baina yao na hata wasio wafrika kutekeleza shughuli rasmi na za kawaida. Katika awamu ya pili, Kiswahili kitumiwe kutekeleza majukumu yote rasmi isipokuwa kortini na katika vyuo vikuu. Ili wafanyakazi wote waweze kupandishwa cheo kazini, walilazimishwa kujua Kiswahili, wafanye mtihani wa Kiswahilina kuupita. Wabunge walilazimika kukijua Kiswahili ndiposawafanikishe mawasilianona wananchi. Vituo mwafaka vya utoaji mafunzo Kiswahili vikajengwa vingi kuwawezesha kupata mafunzo ya Kiswahili.

Mwaka wa 1974, kifungu cha 53 cha katiba kuhusu lugha kilifanyiwa marekebisho. Kiswahili kikawa lugha rasmi badala ya Kiingereza. Watu wakachanganyikiwa kwani walikuwa wafanye mtihani wa Kiingereza badala ya Kiswahili. Hali hii ilipelekea marekebisho ya kifungu hicho 1975 ndipo Kiingereza na Kiswahili zikawa lugha rasmi nchini Kenya.

Kiswahili kikiwa kinatumika kuendeleza mijadala ya bunge tu lakini kuandikia ripoti za bunge Kiingereza ndicho tu kilikuwa kikitumika. Hali hii ufikia 1979 katika uongozi chini ya mzee Moi ambapo mjadala wa kila mbunge alitakiwa kujua Kiswahili. Kinyume na ilivyokuwa hapo awali wakati Katiba iliwahitaji wabunge kujua Kiingereza tu. Mjadala huu ulipelekea marekebisho ya kifungu 53 cha katiba na kupelekea wabunge kujifunza Kiswahili na Kiingereza. Kwa sababu ya ukosefu wa rasilimali na mikakati ya kutekeleza wajibu huo, hali hiyo ilizindikana. Katiba ya wakati huo kifungu 92 kilisema kuwa watu ambao si wa Kenya na wangependa kuwa raia wa Kenya walitakiwa kujifunza Kiswahili. Hapo Kiswahili kilipata hadhi mpya ambapo wabunge pia walianza kuitumia kupigia siasa na kuwasiliana na wananchi. Lugha hii ya Kiswahili ilianza kutumika bungeni kuendeleza mijadala ya Kiswahili na Kiingereza.

Hadhi mpya ya Kiswahili imetokana na katiba ya Kenya ya 2010. Katika sura ya pili kifungu nambari saba(7) na ibara ya (ii) ,lugha rasmi zinatambuliwa sasa zikiwa ni Kiingereza na

kiswahili. Katika katiba hii ya 2010, sura ya nne(4) kifungu cha 120 ibara (v) lugha rasmi za bunge zimetambuliwa kama Kiswahili, Kiingereza na lugha ishara. Shughuli zote za korti huendeshwa kwa Kiingereza na kiswahili. Kiswahili hutumiwa katika mahakama za chini hasa vijijini na panapopatikana mkalimani hutafsiri Kiingereza kwa Kiswahili. Hata hivyo, lugha ya kuandikia ripoti kortini ni Kiingereza. Wakati baada ya kipindi cha ukoloni, Kiswahili kimepokelewa kwa njia chanya. Hii inaonekana kutokana na namna lugha hii ya Kiswahili inatumiwa. Kufikia sasa, Masuala ya Kijamii yanayohusiana na stakabadhi kama vyeti vya kuzaliwa, kufa na pasipoti katika uhamiaji vinaweza kutafsiriwa kwa Kiswahili. Magonjwa ya zinaa kama vile Ukimwi na wizara za kilimo, ufugaji na wanyama zinaweza kufasiriwa kwa Kiswahili hata katika idara ya polisi, Kiswahili hutumiwa katika mawasiliano. Kwa mujibu wa mbaabu (1996), wakuu wa wilaya, Machifu, manaibu wa Chifu, wawakilishi wa wadi mara nyingi hutia Kiswahilikuwasiliana na wananchi hasa vitongojini ambapo wananchi wengi hukifahamu Kiswahili kikilinganishwa na Kiingereza. Vijana wengi hutumia Kiswahili. Hata hivyo, wanakiangamiza sana kwa kutumia Sheng'

#### **2.2.6 Vyombo vya habari**

Vyombo vya habari husaidia kuelimksha na kuburudisha wananchi hasa wa mashinani ambao hufahamu Kiswahili kuliko Kiingereza. Taarifa za habari hupeperushwa kwa Kiswahili katika redio mfano: Idhaa ya taifa, Redio citizen, Redioambo, Qfm na Redio Maisha. Televisheni pia huonyesha vipindi tofautitofauti kwa Kiswahili. Baadhi ya televisheni kama vile runinga ya KTN, NTV, K24, runinga ya Citizen hupeperusha habari jioni na asubuhi kwa Kiswahili. Magazeti kama vile gazeti la taifa leo ambalo ni la pekee linaloandikwa kwa Kiswahili huchapishwa na ujumbe kama nukuu za kila wiki, mashindano ya uandishi wa insha tofauti, jamvi la kisiasa na sokomoko la machapisho ya mashairi na masuala ya spoti.

Vyombo vya habari pasi na kuendeleza Kiswahili vimekidunisha Kiswahili kwa njia moja au nyingine kwani baadhi ya vipindi hupeperushwa kwa ukiushi mkubwa wa sarufi ya Kiswahili. Kwa mfano vipindi ka vile kipindi cha Papa Shirandula, Maria, Zora, Sultana, Aziza na baadhi ya vipindi kama vile futuhi huchezwa pasi na kuzingatiwa sarufi za Kiswahili na hivyo kukidunisha. Hali hii huibua mielekeo hasi kuhusu Kiswahili kwa wafanyakazi wa hali ya chini na kuona Kiswahili kama lugha ya watu wa hadhi ya chini.

Serikali ya Kenya baadaye ilianza kuchukua hatua ya kuimarisha Kiswahili. Kenya ambayo ni jamii ya wingilugha ina lugha takriban arobaini (40) zizungumzwa na watu wa makabila tofauti Abdulaziz (1982). Kiswahili kilichukuliwa na kupandishwa hadhi na katiba ya Kenya ya 2010 kama lugha rasmi. Hivyo kinaweza kutumiwa kutekeleza majukumu rasmi. Kiswahili kama kilivyo Kiingereza, lugha ishara na breli ni lugha ambazo kikatiba zinaweza kutumiwa katika mazingira rasmi. Kulingana na Jamuhuri ya Kenya (2013:28), jitihada zinapaswa kufanywa za kuunda mikakati ya kuwahakikishia Wakenya kuwa wamebadilisha mtindo wa kukitumia Kiingereza katika mazingira rasmi na kukitumia Kiswahili sawia na Kiingereza katika mazingira maalum ya kiafisi na asasi za kielimu Jamuhuri ya Kenya (2013:25).

Kama zilivyotajwa katika katiba ya Kenya, lugha za kienyeji zitalindwa kulingana na inavyoelezwa katika Azimio-Bia la haki za matumizi ya lugha UNESCO (1998). Kwa mujibu wa maelezo haya serikali ya Kenya inapaswa kuhakikisha mikakati ya kuhakikisha kwamba wananchibwa Kenya wanatumia lugha wanayoifahamu na kuelewa hali na wakati unapobidi Jamuhuri ya Kenya (2013:12). Kama ilivyoeleza kuwa, katika elimu ya kitengo cha msingi cha darasa la kwanza litolewe kwa lugha inayozungumzwa katika eneo la shule. Jamuhuri ya Kenya (2013:23). Kwa sababu hii serikali inapaswa kuchukua hatua ya kuunda kituo cha ufundishaji Kiswahili kama lugha geni na ya kutahiniwa hapa nchini Kenya. Vilevile, serikali ibuni mitindo ya lugha ishara, breli na watu wenye changamoto za ulemavu wa kimaumbile kitaifa ili itumiwe kuwafundisha maadamu ndiyo lugha ya kwanza ya watu hao Adoyo (2002:89). Hatua hii itaondoa mielekeo hasi kuhusu Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa Kiswahili.

### **2.2.7 Hitimisho**

Historia ya mielekeo ya lugha ya Kiswahili katika kipindi cha ukoloni wa mzungu Kenya inaonyesha kwamba kulikuwa na mielekeo hasi na chanya kuhusu lugha hii na kwamba mielekeo hii ilitegemea faida na hasara ambazo wadau walitegemea kupata. Wakoloni watawala walilazimika kuwa na mielekeo hasi pale ambapo walikiona Kiswahili kama kifaa hatari kwa usalama wao na wakawa na mielekeo chanya kwacho pale ambapo waliona na kuhisi kwamba kingewasaidia kwa mfano katika vita. Kwa upande mwingine wamisheni walikuwa na mielekeo hasi kuhusu Kiswahili pale ambapo walikifungamanisha na dini kinzani na pinzani ya kiislamu na wakati huo huo wakawa na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili pale ambapo kiliwarahisishia kazi yao ya mahubiri ya injili. Wakenya nao kama wadau walikuwa na mielekeo hasi kuhusu



Kiswahili ilipokuwa kwa swala la ajira lakini wakawa na mielekeo chanya kukihusu pale kilipowaunganisha kama watu wamoja. Kimsingi kipindi cha ukoloni wa Mzungu Kenya kilikuwa na Mielekeo hasi na chanya kuhusu Kiswahili.

Sura hii imekuwa sura ya msingi katika utafiti wetu. Katika sura ifuatayo tumechambua data tuliyoikusanya kuhusiana na mada yetu ya utafiti na kujadili mielekeo ya wakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa.

## **SURA YA TATU**

### **3.0 MIELEKEO YA WAKUU NA WAHADHIRI WA CHUO KIKUU CHA NAIROBI KUHUSU KISWAHILI**

#### **3.1 Utangulizi**

Tumejadili historia na maendeleo ya Kiswahili nchini Kenya katika sura ya pili.. Sura hiyo ilionyesha namna Kiswahili kilitumiwa katika miada tofauti ya kielimiu, vyombo vya habari, wakati na baada ya ukoloni. Katika sura ya tatu tumejadili mielekeo ya wasimamizi wakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa na athari zake. Kiswahili na Kiingereza ni lugha mbili rasmi nchini Kenya. Tunalenga kubaini namna lugha hizi mbili zinavyotumiwa katika miktadha rasmi nchini Kenya katika miada rasmi tofauti na jinsi zinavyotekeleza majukumu yake.

Kukubali au kutokubali kwa watafitiwa kuhusiana na Kiswahili kama lugha rasmi kumeangaziwa katika sura hii. Hivyo basi, matokeo ya utafiti wetu yatakuwa ya muhimu kwani yatawapa mwelekeo na kuwaongoza wapangaji lugha kukipa Kiswahili nafasi yake kama lugha rasmi

kutekeleza majukumu rasmi chuoni na katika taifa la Kenya kama inavyotarajiwa baada ya kupewa hadhi hii na katiba ya Kenya ya 2010. Tumetumia vigezo mbalimbali katika uchanganuzi wa data ili kubaini namna matumizi ya Kiswahili yalivyo katika Chuo Kikuu cha Nairobi kulingana na mtazamo wa upangaji lugha kihadhi. Vigezo hivi ni kama vile umri, jinsia na viwango vya elimu ambavyo vilizingatiwa kuwatafiti walengwa wetu ambao ni wakuu wa idara, wasimamizi wa vitengo vya idara, wahadhiri ambao ni madaktari na maprofesa walitafitiwa.

Utafiti huu umefanwya katika Chuo Kikuu cha Nairobi katika idara za Lugha na Mawasiliano, Soshiojia, Anthropolojia, Fasihi ya Kiingereza, Jiografia, Historia, Diplomasia na Maktabani. Tumetumia mbinu ya mahojiano, hojaji na uchunzaji. Hii ni kutokana na maelezo ya Ajzen na Fishban (1980) kuwa ili kuelewa mielekeo ya watu, sharti utathmini kinachosababisha mielekeo hiyo kwa kuipima kupitia mbinu mbalimbali kama hojaji na mahojiano. Mtafiti basi alitumia hojaji na mahojiano ili kuifahamu mielekeo yao. Data ilikusanywa kwa kutumia hojaji likati yenye maswali yaliyolenga Kiswahili kinavyotumiwa katika Chuo Kikuu cha Nairobi kama lugha rasmi na ya taifa.

### **3.1.1 Matokeo ya Utafiti**

Utafiti wetu ulilenga watafitiwa ishirini na saba kutoka kwa hamsini na wawili. Ili kupata mielekeo ya wakuu na wakufunzi wa Chuo Kikuu cha Nairobi kuhusu Kiswahili katika utekelezaji wa majukumu rasmi. Tulihitaji kujua Kiswahili kinavyotumiwa chuoni pamoja na lugha zingine na kinavyochukuliwa katika idara zingine: Kiingereza, Kichina, Kikorea, Kiarabu na Kijerumani. Hatukuhoji wahadhiri na wakuu wa idara ya Kiswahili kwani kulikuwa na uwezekano wa kutupa mielekeo chanya. Wahadhiri 17 (asilimia 58%) na wasimamizi wakuu 10 (35%) walihojiwa. Wahadhiri 15 (51%) walipendelea kujaza hojaji kwa lugha ya Kiingereza na wawili (6%) ndio waliopendelea kujaza kwa Kiswahili. Wasimamizi wakuu wote 10 (35%) walijaza hojaji kwa Kiingereza.

Jinsia ya kike na kiume zilitafitiwa katika suala zima la ujazaji wa hojaji kwa kutumia lugha rasmi za Kenya. Wahadhiri 6 wa kike (50%) na wahadhiri 9 wa kiume (33%) walitafitiwa. Katika jinsia ya kike, wahadhiri wote 75% walipendelea kujaza hojaji kwa Kiingereza na wale wa kiume asilimia 48% walipendelea kutumia Kiingereza kujaza hojaji na walimu wawili 2 ((6%) walipendelea kujaza hojaji kwa Kiswahili. Wasimamizi wakuu wote waliotafitiwa 10 (35%) walijaza hojaji kwa Kiingereza. Kuwatafiti walengwa wetu tukizingatia kigezo cha jinsia

kulitusaidia kujua iwapo kuna mielekeo inayotokana na watawala wakuu na wahadhiri kwa misingi ya kijinsia. Kulingana na Giles (1982) kundi ndani likigudua lugha yake ni ya hadhi ya chini linaweza kujihisha na kundi nje ili liweze kukubalika na kujitambulisha na kundi hilo. Katika hali hii watawala wakuu wenye umri mkuu walitawaliwa na maswala ya kihistoria ambapo Kiswahili hakikuwa lugha ya lazima na lugha ya watu wasiosoma na wa hadhi ya chini. hawakukionea Kiswahili fahari wakakiona kuwa hakina maana hali ambayo inajitokeza katika Chuo Kikuu cha Nairobi mpaka leo inayosababisha mielekeo hasi. Hali hii inadhihirishwa na kielelezo hiki cha lugha walivyopendelea kujazia hojaji.

**Kielelezo 1: Upendeleo wa Lugha ya Kujaza Hojaji wa wahadhiri na watawalawakuu**

<b>Wahadhiri na wakuu</b> <b>Lugha</b>	<b>Wahadhiri wa kike</b>	<b>Wahadhiri wa kiume</b>	<b>watawalawakuu</b>	<b>Jumla</b>
<b>Kiswahili</b>	0 (0%)	2 (6%)	0(0%)	2 (6%)
<b>Kiingereza</b>	6 (50%)	9(33%)	10(35%)	92%
<b>Asilimia</b>	6%	11%	10%	100%

(Chanzo za takwimu hizi ni utafiti huu)

Katika suala la umri, asilimia 75 ya wahadhiri ni wa miaka baina ya 30 na 60. Katika watafitiwa hawa, hakuna aliyekuwa na umri chini ya miaka thelathini. Watawalawakuu wengi(asilimia

80%) walikuwa na umri wa miaka 48 na kuendelea. Wahadhiri wasaindizi ndio waliokuwa na umri wa miaka kati ya 30 na 40. Kwa jumla hawa walikuwa watatu (11%). Pia kulikuwepo wahadhiri watano (19%) walikuwa na umri wa zaidi ya miaka 60 na wasimamizi wakuu 6 (22%) na ambao walikuwa na umri wa zaidi ya miaka 65.

Katika kujaza hojaji, wahadhiri waliokuwa na miaka kati ya 30- 40 ndio walipendelea kujaza hojaji kwa Kiswahili. Wengine walipendelea Kiingereza.

Kutokana na kigezo hiki cha umri, tumebaini kuwa watafitiwa wenye umri mkubwa wameathiriwa na maswala ya kikoloni ambapo watu walikuwa wanakandamizwa kutumia lugha za kigeni na kupewa adhabu wakitumia Kiswahili. Kulingana na watafitiwa wetu wenye umri mkubwa hali hiyo iliwafanya wakakichukia Kiswahili hata Kazini mpaka leo. Giles (1982) anaeleza kuwa watu wa kundi ndani wanapogudua kuna adhari ambazo hazivasaidii wanahamia lugha ya kundi nje ambalo watatumia mbinu zao kama vile kujifunza lafudhi yao ili waweze kukubalika na kundi hilo ili waonekane bora zaidi. Hali hii iko wazi kwa watafitiwa wetu wenye umri mkubwa huku wenye umri mdogo wakipendelea Kiswahili kwa vile wamekikpata kama lugha ya taifa na kuonyesha mielekeo chanya.


**Kielelezo 2 : Lugha ya Kujaza Hojaji kiumri**

Umri \ Lugha	Kiswahili			Kiingereza		
	Idadi	Asili	Digrii	Idadi	Asili	Digrii
<b>Kati ya miaka 30-40</b>	3	11	40	2	7	27
<b>Kati ya miaka 41-50</b>	9	33	120	6	22	80
<b>Kati ya miaka 51-60</b>	5	19	67	9	33	120
<b>Miaka 60 na zaidi</b>	10	37	133	10	37	133

<b>Jumla</b>	27	100	360		100	360
--------------	----	-----	-----	--	-----	-----

**Chati 1 .Uchanganuzi wa data ya walengwa.**

### Tulichanganua walengwa kwa kutumia paichati (umboduara)



#### 3.1.2 Mielekeo ya wakuu na wahadhiri

Uchanganuzi wa data hii umefanywa kwa kuzingatia malengo mbalimbali.

Watawalawakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi walihojiwa kwa kuulizwa watoe maoni yao yanayohusu Kiswahili kama rasmi na lugha taifa Kenya. Asilimia 85% walionyesha mielekeo chanya kuhusiana na namna Kiswahili hutekeleza majukumu yake kama lugha ya taifa. Kunao watafitiwa wengine wapatao asilimia 15% walionyesha kutokuwa na msimamo kamili wa Kiswahili kama lugha ya taifa.

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa baadhi ya wahadhiri na wasimamizi wakuu wa Chuo Kikuu cha Nairobi walionyesha mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi.

Wahadhiri 11(40%) walionyesha ukubalifu wao kuwa kiswahili ni lugha rasmi. Hii ni idadi iliyowakilisha wahadhiri 11 kutoka kwa 27. Hawa ni wale waliokuwa na umri wa miaka 30-45. Baadhi ya wale walikataa kujaza hojaji kwa Kiswahili walionyesha mielekeo hasi walipohojiwa. Wengi wao (idadi) ni wa jinsia ya kike. Baadhi yao walipendelea Kiingereza. Maoni yao ni kwamba Kiswahili huwa kigumu sana katika kuandikia na kufundishia. Kulingana nao, kuzungumza kwa Kiswahili sanifu na ufasaha wa kusema kwa Kiswahili si rahisi. Mara nyingi wao hulemewa na matamshi na hivyo kukitumia Kiswahili katika mianda rasmi ni kugumu. Wao walidai kuwa kukitumia Kiswahili katika mawasiliano ya kawaida na kukipendelea Kiingereza

katika shughuli rasmi za idara, mikutano na shughuli za uandishi. Hapa wahojiwa wa jinsia ya kike wamedhihirisha hali ya mwachano ambayo inawafanya wawe kundi maalum kivyake na la kipekee kama anavyosema Giles (1992)

Wahadhiri na wakuu wa idara za Kichina, Kireno, Kikorea, Kiarabu walipendelea kutumia Kiingereza. Baadhi ya waliopendelea kutumia Kiswahili ni wa idara ya Isimu na Mawasiliano, wa Saikolojia, Anthropolojia, Sosholojia na Kiarabu. Kutokana na hali hii tunaweza kusema kuwa hawa ndio walioonyesha mielekeo kubalifu kuhusiana na Kiswahili ja lugha rasmi. Hata hivyo, tukiangazia utendaji Kiswahili katika kuendeleza shughuli za chuo, huwa wanakitumia kwa kukichanganya na Kiingereza. Watafitiwa kumi na sita kutoka kwa ishirini na saba wailionyesha mielekeo chanya kuhusu Kiingereza kama lugha rasmi. Katika mahojiano ya kama kuna umuhimu wa kudumisha utumizi wa lugha za kigeni kama Kiingereza nchini Kenya, wahadhiri 16 kutoka kwa 27 ambao ni kiwakilishi cha asilimia 59% walionyesha mielekeo chanya kuhusu Kiingereza. Wao walieleza kuwa, nimuhimu kuendelea kutumia Kiingereza ja lugha rasmi. Kwa maoni yao, japo kuna lugha mbili rasmi nchini Kenya watu wengi, hupendelea Kiingereza kwani ndiyo lugha ambayo ina mashiko makubwa na iliyofahamika na watu wengi. Walieleza kuwa kuna uwezekano kuwa wengi hasa katika maofisi ya umma hawajui kama Kiswahili ni lugha rasmi bali wanakitambua tu kama lugha ya taifa. Sampuli iligawika katika makundi ya jinsia, umri, kiwango cha elimu kwa watafitiwa wetu, wahadhiri na wasimamizi wakuu katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kijinsia, wanawake wote walipendelea kutumia Kiingereza katika mianda rasmi na kutumia Kiswahili katika mazungumzo ya kawaida. Wanawake 6 ambao ni asilimia 50% walipendelea Kiingereza kuwa lugha rasmi na Kiswahili katika mianda ya kutekeleza shughuli za kitaifa au za kawaida. Wahadhiri wa jinsia ya kiume 4(26%) walikuwa na mielekeo ambayo ni chanya kuhusiana Kiswahilina hadhi yake kama lugha rasmi. Suala la kijinsia linasadifu kuwa, wanawake wachache wanapendelea kutumia Kiswahili kama lugha rasmi ilhali wanaume wengi wakipendelea Kiswahili. Katika hali hii, wanawake wote hawakupendelea Kiswahilikama lugha rasmi na Kiswahili kutumika kuendesha shughuli za kawaida. Kama ilivyodhihirika hapo juu wanaume wamejitokeza kama kundi ndani inapokuja katika matumizi ya Kiswahili huku wanawake wakijidhihirisha kama kundi nje na haya ndiyo yaliyomo katika nadharia ya Giles (1982) ya makutano na mwachano.

### Kielelezo 3: Matumizi ya Kiswahili kama Lugha Rasmi

<b>Mielekeo</b>	<b>Mielekeo chanya</b>	<b>Mielekeo hasi</b>	<b>Jumla</b>
<b>Jinsia</b>			
<b>Kike</b>	6 (50%)	0 (0%)	6 (50%)
<b>Kiume</b>	4(26)	2 (13%)	6 (50%)
<b>Jumla</b>	10 (83%)	2 (13%)	12(100%)

Baadhi ya watafitiwa wa jinsia ya kiume hawakuonyesha msimamo wao wa kukipendelea au kutokukipendelea Kiswahili. Baadhi hawakurudisha hojaji kama njia mojawapo ya kujisemea mielekeo na misimamo yao ya kilugha katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Kulingana na Giles (1982) jamii yenye watu wa makundi mawili ambayo ni ya hadhi ya juu na hadhi ya chini kundi la hadhi ya chini linaweza kujitambulisha kwa kutumia lugha ya kundi la hadhi ya juu ili lionekane bora pia. Giles (1992) anasema kuwa wanaohamia lugha ya wenzao ni kundi ndani na wanaojitambulisha na lugha yao ni kundi nje. Katika data yetu watu wa umri mkuu ambao walionyesha mielekeo hasi kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi ni ndio kundi nje na wenye umri mdogo ni kundi ndani kwa kujitenga na Kiswahili kama lugha rasmi kukipendelea kama lugha ya taifa na kuibua ukundi ndani na ukundi nje kama anavyosema Giles (1982).

#### **Matumizi ya Kiswahili Kiumri**

Katika kitengo cha umri, wahadhiri wa kiume wenye umri wa miaka 30- 40 waliotafitiwa walionyesha kuwa na mielekeo chanya ya kutumia Kiswahili ikiwa lugha rasmi. Wale wa umri wa miaka hamsini kuendelea, walionyesha mielekeo hasi kuhusiana na matumizi ya Kiswahili katika mianda rasmi kutekeleza shughuli rasmi. Walionyesha mielekeo chanya kwa kiasi kikubwa kukitumia Kiswahili ja lugha taifa. Mielekeo hii ilisababishwa na masuala ya kihistoria ambapo katika miaka ya ujana wao Kiswahili hakikuwa cha lazima nchini Kenya na wala hakikutahiniwa katika mfumo wa elimu kama somo la lazima. Hivyo hawana uelewa wa Kiswahili kama kiingereza iliyokuwa imefanywa ya lazima na Wakoloni upendeleo wa lugha moja katika utenda kazi kama huu ndio Giles (1982) anaoueleza kwamba unaweza kusababisha mielekeo hasi katika matumizi ya lugha moja miongoni mwa lugha zingine kama inavyodhirika hapa kwa watafitiwa wetu.



**Kielelezo 4: Matumizi ya Kiswahili Kiumri**

<b>Umri</b> <b>Lugha</b>	<b>30- 40</b>	<b>41-50</b>	<b>51-60</b>	<b>60 na zaidi</b>	<b>Jumla</b>
<b>Kiswahili- lugha rasmi</b>	4 (14%)	1 (3%)	0(0%)	0(0%)	5 (18%)
<b>Kiswahili- lugha taifa</b>	2(7%)	9(33%)	7(25%)	4(14%)	27(100%)
<b>Jumla</b>	6(21%)	10(36%)	7(25%)	4(14%)	96%

Kwa kuzingatia suala hili la umri inabainika kwamba watu wa umri mchanga wanajitenga kama kundi maalum na kwa hiyo kunakuwa na hali ya ukundi ndani tofauti na wale wa umri mkubwa ambao wanaonyesha hali ya ukundi nje kama anavyosema Giles (1982) katika nadharia yake kuwa kundi ndani linapojitenga na kutumia lugha yake kujitambulisha huwa kunaibuka makutano na ambapo kundi ndani huacha lugha yao na kuiona duni na kuiacha na tamaduni zake kujifunza lugha ya kundi nje kujitambulisha nayo huwa kumetokwa mwachano. Hali hii inadhihirika wazi kama inavyoonekana katika jedwali hili namna watafitiwa wetu wanavyokikumbatia Kiswahili ja lugha rasmi na taifa.

**Kiwango cha elimu**

Viwango vya elimu vya watafitiwa wetu vilikuwa vya aina zifuatazo: Profesa, profesa washiriki, madaktari wandamizi na wanaosimamia mihadhara chuoni. Katika kitengo hiki, tuliwahoji maprofesa 3 (60%), madaktari wandamizi 9(52%), na wahadhiri 3(60%). Kati yao, maprofesa walikuwa na mielekeo kubalifu katika namna Kiswahili kinavyotumiwa ja lugha rasmi. Madaktari waandamizi watano (60%) walionyesha umuhimu wa Kiswahili kama lugha rasmi. Wahadhiri wote walionea fahari Kiswahili kikitumiwa ja lugha rasmi. Maoni yao ni kuwa kuna umuhimu wa Kiswahili kutumiwa kama lugha rasmi kutekeleza majukumu rasmi.

Majibu kutokana na kipengele cha kiwango cha elimu ni kama yanavyojitokeza katika kielelezo hiki na kinachotokana na majibu hayo ya matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi nay a taifa: -

**Kielelezo 5: Kipengele cha kitengo cha elimu**

<b>Lugha Kitengo</b>	<b>Kiswahili-Lugha Rasmi</b>		<b>Kiswahili- Lugha Taifa</b>	
	<b>Idadi</b>	<b>Asilimia</b>	<b>Idadi</b>	<b>Asilimia</b>
Maprofesa	3	6	0	0
Madaktari	5	29	4	23
Wahadhiri wasaidizi	3	6	0	0
Jumla	11	41	4	23

Siala hili la viwango vya elimu limeonyesha kwamba watu waliosoma wanayo mielekeo inayofanana kuhusiana na matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi. Hapa hivi kuna hali ya makutano kama inavyokariri nadharia ya Giles (1982)

Baadhi ya maprofesa na madaktari walieleza kuwa huwa wanaelewa Kiswahili lakini hawakitumii katika mawanda ya elimu. Hii ni kutokana na kukosa kujua baadhi ya tafsiri za misamiati ya kutumia katika kazi za kimaandishi idarani na kutojua Kiswahili sanifu. Kutokana na watafitiwa wetu, watafitiwa wenye umri mdogo walionyesha mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kama lugha

rasmi na matumizi yake kama lugha ya taifa.Hii ni kutokana na hali kwamba wamekisoma katika umri wao mdogo shule za upili na za msingi.Wale waliokuwa na umri mkubwa walionyesha mielekeo hasi kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi lakini wakaonyesha mielekeo chanya kukitumia Kiswahili kama lugha ya taifa.Hili lilitokana na hali kwamba kuna mielekeo iliyotokana suala la kikoloni ambapo Kiswahili kilionekana lugha ya wasiosoma.Hali hii inaibua mielekeo kati ya waliosoma na wasiosoma kutokipendelea kijitambulisha kwa Kiswahili na kuonekana kama wa hadhi ya chini.Hili ndilo Giles(1982) analosema kuwa kundi ndani linapendelea kujiunga na kundi nje kama makundi maalum kutokana na vile watafitiwa wetu wanavyodhihirisha kupendelea Kiswahili kwa wale wenye elimu kubwa ya matumizi ya lugha na wenye elimu dogo.

### **3.1.3 Mielekeo ya Wasimamizi wakuu**

Katika kipengele hiki, tuliwatafiti viongozi wa idara tofauti za chuo, tukilenga wenyekiti wa idara tofauti na wasimamizi wa idara na vitengo. Tuliweza kuwahoji wenyeviti katika idara 5(35%) na wasimamizi wa idara na vitengo kutoka idara 8 (57%) na katika jumla hiyo, wenyeviti wote walionyesha kuelewa kuwa Kiswahili ni lugha rasmi lakini katika uendeshaji wa shughuli za idara huwa wanatumia Kiingereza. Vilevile, wasimamizi wote wa idara, hawakupendelea kutumia hojaji za Kiswahili. Maelezo yao yalikuwa kuwa mara nyingi wana washiriki wengine katika idara wasiofahamu Kiswahili. Vilevile, wao hawana msamiati wa kutosha wa kuandikia sheria za utekelezaji wa shughuli za chuo kwa Kiswahili. Hivyo basi, waliungama kuwa wao wanabakia kutumia Kiswahili katika maongezi ya kawaida.Ukawaida huu unatokana na manufaa ya lugha wanazozitumia.Lugha inayotumiwa sana katika maeneo ya kazi na ajira ndiyo wanayoipendelea kuitumia.Giles (1982) anaeleza kuwa watu wa kundi ndani na kundi nje hupendelea lugha inayowasaidi kujiendeleza kiuchumi kama inavyojitokeza kwa watafitiwa wetu kupendelea lugha inayowafanikisha kuendesha shughul za kazi na ajira bora.

**Kielelezo 6: Mielekeo ya watawala wakuu wa Chuo kuhusu kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa**

watawalawakuu Lugha	Wenye kiti	Wakuu wa idara	Jumla
<b>Kiswahili-lugha taifa</b>	5 (35%)	8 (57%)	92%
<b>Kiswahili-lugha rasmi</b>	0(0%)	0(0%)	0(0%)
<b>Jumla</b>	5 (35%)	8 (57%)	92%


Hao wasimamizi wa idara na vitengo mbalimbali vya chuo wameonyesha kuwa wao ni kundi moja na kwa hivyo kuna hali ya makutando katika matumizi yao ya lugha wanapotekeleza shughuli zao. Kwa hali hii wanakiacha Kiswahili na kukikumbatia Kiingereza kama lugha ya kazi. Matokeo ya utafiti huu, yametubainishia kwamba Kiswahili kimekubaliwa na baadhi ya wakuu na wasimamizi wa Chuoni huku Nairobi kama lugha rasmi na ya taifa. Hata hivyo, lugha hii haitumiki katika utekelezaji wa majukumu rasmi. Hii inamaanisha kuwa urasmi wa Kiswahili haujatambuliwa katika utendaji wa majukumu rasmi.



Matokeo haya yanadhihirisha kuwa kuna zaidi ya kile kisemwacho katika katiba na mielekeo ya watu wanaotekeleza kile kinachosemwa katika katiba ya Kenya. Kwa hali hii pale ambapo tungetegemea kwamba kuwe na makutano kilugha kumejitokeza mwachano kwa sababu ya shughuli zinazotekelezwa na watafitiwa hawa.

**Mukhtasari wa vipengele vilivyotafitiwa**

lugha vipengele	Kiswahili kama lugha rasmi	Kiswahili kama lugha taifa

	idadi	Asilimia %	Degree <sup>(0)</sup>	idadi	asilimia	Degree <sup>(0)</sup>
<b>Tofauti za kiumri</b>	15	34	123	12	19	68
<b>Kiwango cha elimu</b>	11	25	90	16	25	90
<b>jinsia</b>	9	20	74	18	28	101
<b>Watawalawakuu</b>	2	5	16	8	13	45
<b>wahadhiri</b>	7	16	57	10	16	56
<b>jumla</b>	44	100	360	64	100	360





Tulitumia nadharia ya Giles (1982) katika uchanganuzi wadata yetu. Kwa kuzingatia mihimili mikuu ya nadharia hii ya makutano na mwachano inadhihirika ambapo japo Kiswahili ni lugha ya kiasili wakuu wanaonelea kuegemea Kiingereza ambacho ni lugha ya kigeni kwa sababu ndio inayokimu mahitaji yao ya kimawasiliano na kazi. Baadhi ya wakuu na waadhiri ni wa kutoka nje ya Afrika mashariki na hawana uelewa mwafaka wa kiswahili. Baadhi ya wahadhiri wamo chuoni kwa sababu ya kufanya ajira zao. Kwa hivyo lugha wanayoitumia ni Kiingereza ili kukidhi na kuhifadhi kazi yao. Mhimili wa makutano (kundi ndani) unadhihirika pale ambapo watu wanakichukulia Kiswahili kwa mielekeo chanya kama lugha ya taifa kama anvyosema Giles (1982). Mielekeo hasi imeleta mwachano na kukitinga Kiswahili kama lugha rasmi inayojulikana na wengi katika idara zao na hivyo kutoitumia kuendesha mikutano wanapokuwa kazini nakuichukulia kama lugha ya kuwasiliana katika mawasiliano ya kawaida tu. Hivyo, wahadhiri wa

Chuo Kikuu cha Nairobi pamoja na wakuu wanakitumia kiingereza kwa wingi kuliko Kiswahili kwa sababu ndicho kinachowapa ajira bora na kukidhi hali nzuri ya maisha yao kama inavyojitokeza katika Nadharia ya Makutano na mwachano ya Giles 1982.

#### **3.1.4 Hitimisho**

Tumeyawasilisha matokeo ya utafiti huu unaohuhusu mielekeo ya Watawala wakuu na Wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi kuhusu Kiswahili ja lugha rasmi na lugha taifa. Katika uchanganuzi wa data hii, matokeo yameonyesha kuwa wakuu na wahadhiri wengi wanapendelea kutumia Kiingereza kuendesha shughuli za idara. Wengi walieleza kuwa Kiswahili sanifu si rahisi kukitumia katika mianda rasmi. Kwa hivyo walionyesha mielekeo hasi kuhusu matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi kuendeleza shughuli za idara chuoni.

Mielekeo hii hasi imetokana na ukweli kwamba shughuli nyingi chuoni hapa hutekelezwa kwa matumizi ya Kiingereza ambayo katika muktadha wa taifa la Kenya ni lugha rasmi ya pili lakini iliyozoeleka na wengi. Kwa hiyo ni swala la mazoea linalopelekea Kiswahili kama lugha rasmi ya kwanza kutotumika kutekeleza shughuli rasmi katika chuo kikuu cha Nairobi. Hivyo basi nadharia yetu imebaini kwamba badala ya kuwa na makutano ya kilugha kwa kurejelea lugha ya Kiswahili kumejitokeza mwachano na haya ndiyo anayosema Giles (1982) katika nadharia yake ya makutano na mwachano kwamba kunakuwa na kundi ndani na kundi nje kwa hiyo badala ya kuwa na kundi ndani kwa Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa Kenya kumejitokeza hawa watafitiwa kama kundi nje wanaojitenga na umma mkubwa wa Wakenya.

## SURA YA NNE

### 4.0 MASWALA YANAYOSABABISHA MIELEKEO KUHUSU KISWAHILI NA ATHARI ZAKE

#### 4.1 Utangulizi

Mielekeo chanya au hasi kwa watafitiwa wetu ilisababishwa na maswala tofautitofauti yakiwemo ya kiuchumi, kihistoria, kijamii na kiisimu. Katika sura hii tumejadili visababishi vya mielekeo kuhusu Kiswahili miongoni mwa watawalawakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa nchini Kenya. Visababishi hivyo vitatoa mwongozo wa watawalawakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi katika upangaji wa lugha na ufanyaji wa maamuzi ya matumizi ya lugha rasmi katika mianda rasmi ya utekelezaji wa majukumu chuoni humo kwa kufuata katiba ya Kenya ya 2010 hasa ikikumbukwa kuwa katiba ndiyo sheria kuu ya nchi yo- yote ulimwenguni hapa.

Katika swali lililouliza: -

- (a) Kuna manufaa ya kukuza, kutunza na kuendeleza matumizi ya lugha ya Kiswahili? Na kufuatiwa na swali hili,
- b. Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

Matokeo yalikuwa kama ifuatayo: -

Maelezo	Idadi ya watafitiwa	Asilmia %
Ndio	22	81
La	5	19



Asilimia 81% ya watafitiwa ilionyesha umuhimu wa kutumia Kiswahili, kukitunza na kukiendeleza. Walikichukulia Kiswahili kama lugha ya kuunganisha wanafunzi, wahadhiri na wakuu wasimamiziwa Chuo Kikuu cha Nairobi na wakuleta utangamano mwema baina yao. Kati ya wakuu wa Chuo Kikuu cha Nairobi waliotafitiwa, kuna wale walionyesha mielekeo hasi dhidi ya Kiswahili kutokana na sababu za kiisimu. Baadhi yao walieleza kuwa, Kiswahili ni rahisi kuongea lakini ni kigumu kukitumia katika maandishi na kutolea hotuba. Hili lilitokana na maoni yao kwamba lugha ya kutumia katika maandishi afisini sharti iwe rasmi na msamiati maalum wa sajili ya afisi mahususi kutumiwa. Kwa mujibu wa maelezo ya watafitiwa husika, lugha sanifu ya Kiswahili na msamiati sanifu si rahisi kupata na hata kutafsiri misamiati hiyo si rahisi. Kutokana na hali hii kama alivyosema Giles (1982), sababu kama hii ya kiisimu huwafanya wasimamiziwakuu wa Chuo Kikuu cha Nairobi pamoja na wahadhiri kuteua na kutumia Kiingereza kuendesha mikutano yao kama inavyoonyeshwa katika swali hili lililoulizwa vile vile:

-

(ii) a. Nayaonea fahari mazungumzo rasmi nikitumia lugha ya Kiswahili badala ya lugha zingine (sema ndio au la)

b. Tafadhali naomba ueleza sababu za jibu lako.

Maelezo	Idadi ya watafitiwa	Asilimia %
Ndio	2	20
La	8	80
Jumla	10	100

Kati ya watawalawakuu tuliowatafiti, asilimia (80%) hawakupendelea kutumia Kiswahili kuendeleza na kuendesha shughuli rasmi au hotuba katika mikutano kwa sababu za kiisimu kama vile Kiswahili sanifu ni kigumu, msamiati wake hutoshi na ni mgumu kuelewa. Aidha, baadhi yao walipendekeza Chuo Kikuu cha Nairobi kichapishe vitabu vingi vya maandishi ya Kiswahili ili kuhamasisha watu wavisome kwa uelewa wa Kiswahili Zaidi Kwa lengo la kupata ufahamu wa lugha hii kwa ajili ya mawasiliano mema.

Baadhi ya wahadhiri waliohojiwa walieleza kuwa ni vigumu kufunzia kozi zingine kwa Kiswahili kwa sababu kutafsiri misamiati ya Kiingereza na lugha zingine kwa Kiswahili ni vigumu. Watafitiwa hawa walisemakuwa baadhi ya misamiati ya kisayansi na kiteknolojia inayopatikana katika lugha nyingine haipatikani kwa Kiswahili.

Baadhi ya watafitiwa walieleza kuwa sababu za kihistoria kama vile mielekeo hasi ya kikoloni iliyoonesha Kiswahili kama lugha duni zilionekana kuwa na mashiko makubwa sana katika kuathiri suala zima la mielekeo dhidi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Kutokana na maelezo yao, lugha wanayoifahamu zaidi ni ile ya kigeni na ambayo hasa ni Kiingereza kilichotumiwa na wakoloni katika enzi za ukoloni. Lugha hii ya Kiingereza ndiyo iliyotumiwa kuandikia vitabu vingi na maandishi mengi kwa ajili ya kubadilisha na hata kukengeusha maisha na fikra za Wakenya waliopata elimu ya Kimagharibi na. Baadhi ya wahadhiri na wasimamiziwakuu waliohojiwawalieleza kuwa katika elimu yao ya msingi, Kiswahili hakikuwa kinatiliwa mkazo sana na hivyo hawakukichukulia kwa umakinifu sana kama lugha ya Kiingereza iliyokuwa ya lazima. Kwa sababu hii wengi wahojiwa waliungama kuwa walichukulia Kiingereza kama lugha muhiimu Zaidi na kukienzi zaidi kuliko Kiswahili. Suala la ukoloni mamboleo katika akili za wasimamiziwakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi lina mizizi yake katika mapuuza ya mafungamano bain ya lugha na utamadunina na kutokuelewa Kiswahili hasa wale wahojiwa wenye umri wa miaka zaidi ya hamsini.

Kutokana na matokeo ya utafiti huu watawala wakuu walipendelea kutoa hotuba zao kwa Kiingereza. Baadhi yao ni wale wenye miaka zaidi ya hamsini walioonekana kuwa hawana Imani na mashiko ya Kiswahili ndani yao kwa madai ya sababu za kihistoria. Watafitiwa wa jinsia ya kike pia walionyesha mielekeo hasi kuhusiana na matumizi ya Kiswahili kutekeleza kazi rasmi za kiofisi chuoni pale. Aidha, hawakupendelea Kiswahili kama lugha rasmi kwa sababu za kiisimu za kutokukifahamu Kiswahili sanifu. Asilimia 59% ya watafiti wailionyesha mielekeo hasi na walioonyesha mielekeo chanya ni kutokana maswala ya utangamano wa kijamii.

Giles (1982) Katika misingi ya kijamii-muundo anaeleza kuwa lugha yenye nguvu zaidi inaweza kunawiri miongoni mwa makundi mengine kihadhi, kiidadi ya watu na mapendeleo ya kiserikali. Kutokana na utfiti wetu Kiswahili hakijapendelewa na watawala wa chuo ila walikipendelea Kiingereza katika kutolea hotuba zao kwa sababu ya kutunza ajira zao. Kutotumika

kwa Kiswahili katika hotuba rasmi ni kwa sababu ya mapendeleo ya Kiingereza ambayo yamekiangamiza Kiswahili kama lugha rasmi.

Uchanganuzi wa matokeo ya utafiti wetu yanadhihirisha kwamba watafitiwa walidhihirisha mielekeo kubalifu kuhusu lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa kuliko matumizi yake kama lugha rasmi kama inayoonyeshwa na swali hili lililowaulizwa: -

(iii) Je, ungependa kutumia lugha ipi unapohutubia wanagenzi katika mikutano inayofanyika nje ya darasa?

Kiswahili

Kiingereza

Kichina

Kikorea

Zinginezo.

Watafitiwa hawa waliombwa vilevile kujibu swali la kufuatilizia lililopo hapa chini.

b. Tafadhali toa sababu za jibu ulilolichagua.

Lugha	Chanya	Asilimia	Hasi	Asilimia	Jumla
<b>Kiswahili</b>	3	18%	14	82%	100
<b>Kiingereza</b>	14	82%	3	18%	100
<b>Kichina</b>	0	0%	0	0%	0
<b>Kikorea</b>	0	0%	0	0%	0
<b>Zinginezo</b>	0	0%	0	0%	0
	17	100%	17	100%	100

Chanzo cha jedwali hili ni majibu waliotoa watafitiwa katika swali la kufuatilia lile la kimsingi.

Kulingana namatokeo ya utafiti huu, Kiingereza ilipata mielekeo chanya mingi. Kulingana na watafitiwa, Kiingereza ndiyo lugha inayojulikana na wadauwengi ambapo katika Chuo Kikuu cha Nairobi wapo waliotoka nje ya taifa la Kenya kama Korea, Uchina, Uarabuni, Ureno, Misri na Ujerumani. Watafitiwa wengi hawakuwa na umaarufu wa kujieleza kwa Kiswahili ikizingatiwa kuwa wametoka katika mataifa ambayo Kiswahili hakizungumzwi. Hivyo, wengi wao hawakupendelea kujaza hojaji kwa Kiswahili. Vilevile asilimia 82% ya watafitiwa hawakupendelea kutumia Kiswahili kuhutubia wanafunzi nje ya darasa. Maelezo yao yalibaini kuwa wengi wao wamo chuoni kwa sababu za ajira na kazi. Lugha iliyowafanikisha kupata ajira ni Kiingereza. Hivyo, wengi waowalichukulia kuwa Kiingereza ndio lugha inayowasaidia kupata ajira bora. Pasi na maingiliano katika taifa, Kiingereza kilichukuliwa nao kuwa lugha ya utangamano wa kimataifa. Walichagua Kiingereza kwa sababu ndio inayowaunganisha na mandhari pana ya ajira bora. Katika hali hii Kiingereza kinachukua nafasi ya maswala yanayokianganiza Kiswahili kama lugha rasmi. Maelezo yaliyotolewa na watafitiwa yanaafikiana na nadharia ya Giles (1982) ya makutano na mwachano kwamba maamuzi ya lugha watu wanayoiteua kuitumia na kujihusisha nayo hutokana na faida wanazopata kutokana na lugha hiyo. Giles (1982) aneleza kuwa wanajamii wa kundi fulani watajihusisha na kundi ambalo lina faida kwao na kujitambulisha nalo. Aidha, katika hojaji, wengi waowalipendelea Kiingereza katika swali la ajira bora kama ilivyodhihirika kwa mujibu wa swali lifuatalo: -

(iv) Ni lugha ipi unafikiri inawezampa mwanafunzi nafasi bora ya ajira nzuri katika siku za halafu?

Lugha	Idadi	Asilimia	Jumla
Kiswahili	6	22	22
Kiingereza	24	58	58

b. Tafadhali eleza sababu?

Katika swali hili, zaidi ya asilimia 50% ya watafitiwa ilichagua Kiingereza nayo asilimia 22% ikapendelea Kiswahili. Watafitiwa wengi walipendelea Kiingereza kwa sababu walikichukulia ndiyo lugha inayotumiwa kuomba kazi, ndio inayotumiwa katika mahojiano na watafitiwa wengi hawajawahi omba kazi kwa kutumia Kiswahili. Kutokana na sababu hii Kiswahilikilionekana kama cha kutekelezea shughuli za kawaida ambazo si rasmi. Kiingereza kilionekana kama kizuizi kilichodidimisha Kiswahili kama lugha rasmi huku kikionekana kuwa lugha bora tangu enzi za ukoloni na kulichukuliwa kuwa lugha ya kutoa ajira bora, kuimarisha uchumi na kuwafanya waonekane kama watu wa tabaka la juu katika mataifa ambayo hayaongei Kiingereza sanakukiwemo Tanzania. Watafitiwa wengi walisema kuwa elimu bora, uchumi na ajira hutokana na lugha rasmi na mashiko iliyonayo kwa wasemaji wake. Baadhi ya watafitiwa walitolea mifano ya kiwango cha elimu ikilinganishwa na vyuo vikuu vya taifa jirani la Tanzania kwa kudaikuwa Chuo Kikuu cha Nairobi kina elimu bora na uchumi imarakwa jumla kuliko vyuo vikuu vya Tanzania vinavyotumia Kiswahili katika shughuli zao nyingi. Hata hivyo, maoni ya watafitiwa wote ni kwamba hatua zichukuliwe ili Kiswahili kitumiwe ofisini kama lugha rasmi kama ilivyotajwa katika katiba ya Kenya (2010) na kama ilivyo katika mataifa mengine ya ulimwenguni hapa.

Swali jingine lililoulizwa watafitiwa lilikuwa: -

(v) Kuna manufaa ya kukitumia Kiswahili na Kiingereza kiusambamba ja lugha mbili rasmi nchini Kenya vyaoni? (Tafadhali jibu ndio au la). Swali la kufuatilia lilikuwa jinsi ilivyo hapa chini: -

b. Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

Maelezo	Watafitiwa	Asilimia %
Ndio	23	85
La	4	15
Jumla	27	100

Watafitiwa asilimia 85% walionyesha mielekeo chanya katika kujibu swali hili. Maelezo yao ni kwamba lugha mbili rasmi ni muhimu kwa sababu kila mtu anaweza kutumia yoyote ile aipendayo wakati anapotekeleza wajibu wake ofisini na idarani. Hata hivyo, wengi kati ya hawa watafitiwawalionyesha kuwa katika hali halisi natumizi, wanaweza kutumia Kiswahili katika mianda isiyokuwa rasmi zaidi kuliko kukitumia kama lugha rasmi. Asilimia chini ya 20% ya watafitiwa ilioonyesha mielekeo hasi katika kujibu swali hili fuatilizi. Walieleza kuwa lugha moja ya kama vile Kiingereza inatosha nainaweza kutekeleza majukumu rasmi. Hali hii inaonyesha kuwa Kiswahili hakina mashiko makuu katika maofisi ya Chuo Kikuu cha Nairobi kama lugha rasmi. Asilimia kubwa inapendelea Kiingereza kuliko Kiswahili katika utekelezaji wa majukumu rasmi idarani na hata nje ya idara mbalimbali za chuoni Nairobi. Mielekeo yao imetokana na hali kwamba ndiyo lugha wanayojua tangu ukoloni, kuwapa ajira bora na hata utangamano wa kimataifa ambapo chuoni mna watu wa kutoka mataifa mbalimbali walioajiriwa na wanaosomea kozi na taaluma mbalimbali. Watafitiwa walionyesha mchango mkubwa uliobainisha kuwa Kiswahili kinaweza kupata nafuu katika matumizi yake kama lugha rasmi chuoni Nairobi. Watafitiwa walieleza kuwa Chuo Kikuu cha Nairobi kinaweza kustawisha matumizi ya lugha za kiasili zinazotumiwa chuoni kama Kiswahili kwa kuzingatia njia kama vile kubuni mikakati itakayohakikisha kuwa Kiswahili kinatumika katika kila idara kutekeleza majukumu rasmi na wakati wa maadhimisho ya sherehe za chuo Kiswahili kitumiwe kuendeshea shughuli za maadhimisho hayo na katika shughuli zingine za chuo. Vilevile katika mitandao ya wanafunzi Kiswahili kitumiwe kutolea matangazo ya kuhamasisha wanafunzi kuhusiana na mambo yanayoendelea shuleni na katika mahojiano yetu ya ana kwa ana na watafitiwa wetu na hata katika uandikaji barua rasmi Kiswahili kitumiwe.

Maelezo ya watafitiwa yalisawiana na maelezo ya nadharia ya Giles(1982) kwamba Kikundi cha chini kinaweza kupigania hadhi ya lugha yao kwa njia ya vyombo vya habari au matumizi ya lugha hiyo shuleni. Hali hii inajidhihirisha kutokana na namna watafitiwa walipendelea lugha mbili rasmi kutumiwa kutekeleza shughuli rasmi. Vilevile wakuu wa Idara ya Kiswahili wanaonyesha juhudi za kupigania lugha ya Kiswahili ili isiondolewe katika idara zingine za Chuo Kikuu cha Nairobi.

Swali lililofuata lilisoma vifuatavyo: -

(vii) Ni changamoto zipi zinazuia Kiswahili kutekeleza majukumu rasmi hapa chuoni Nairobi

<b>Idadi</b>	<b>Majibu</b>
6	Kupendelewa kwa Kiingereza.
2	Kiswahili sanifu ni kigumu.
8	Kiswahili huchukuliwa kama lugha ya kawaida.
3	Hakuna vitabu vingi vya Kiswahili
2	Mielekeo hasi ya kikoloni inayokiona Kiswahili kama lugha duni

Watafitiwa walioulizwa swali hili walionyesha changamoto anuwai. Kwa mfano, watawalawakuu wa chuo wanaohusika na kufanya maamuzi ya uteuzi wa lugha inayotumiwa katika utekelezaji wa majukumu rasmi chuoni, hupendelea Kiingereza zaidi ya lugha zingine licha ya kuwa kuna lugha kadhaa zinazofundishwa chuoni hapa Nairobi zenye wazungumzaji wake kama vile Kikorea, Kichina, Kiarabu, Kiswahili na Kireno. Wakati wa kuandika nyaraka idarani Kiswahili hakipewi nafasi sawa na lugha rasmi ya Kiingereza. Katika kila hali, Chuo Kikuu cha Nairobi husisitiza kazi za maandishi mengi kufanywa kwa Kiingereza. Hata matbaa ya kuchapisha vitabu katika Chuo Kikuu cha Nairobi hakikuwa kinapendelea uchapishaji wa miswada ya Kiswahili kama baadhi ya watafitiwa katika utafiti huu walivyongama. Sheria kama hii huangamiza na kuua Kiswahili katika utendakazi wake chuoni Nairobi. Mhojiwa huyu alipendekeza kuwa chuo kiwe kinaendeleza shughuli zake rasmi kwa Kiswahili hasa katika idara zingine. Kwa maoni yake, sheria ya kutochapisha vitabu vya Kiswahili ihaririwe na kuandikwaupya ikionyesha ni majukumu yepi Kiswahili na Kiingereza zitakuwa zikitekeleza kwa usawa chuoni. Vitabu vya Kiswahili viweze kuchapishwa na matbaa ya Chuo Kikuu cha Nairobi. Pia mtafitiwa huyu alipendekeza kuwa stakabadhi zingine kama vile vyeti vya kufuzu, vitambulisho vya wanafuzi, stakabadhi za kufanyia mitihani, kadi za mitihani na orodha ya majina ya kufuzu ziandikwe kwa Kiswahili.

Giles (1982) alieleza kuwa mapendeleo ya lugha ya kundi moja yanaweza kusababisha kunawiri kwake hasa kwa kundi hilo na kutinga makundi mengine. Aidha kulingana na Giles (1982) kundi ndani ambalo ni la chini linaweza kujinasua kwa kupigania lugha yao kwa kuangazia mipaka

iliyopo kati ya kundi lao na kundi la juu na kuifunga kwa kujiunga na kujinasibisha nayo kama inavyodhihirika hapo juu kwa watafitiwa wetu.

Giles (1982) anafafanua kwamba kundi ndani linaweza kupigania lugha yao kwa mbinu mbalimbali kama vile vyombo vya habari, redio na njia zingine. Kwa hali hii watafitiwa wetu walionyesha mapendekezo yanayoonesha mikakati mbalimbali ambayo Chuo Kikuu cha Nairobi inapaswa kuchukua ili kuokoa Kiswahili kama lugha rasmi ya taifa. Hivyo wahojiwa walieleza kuwa watu wahimizwe kutumia lugha sanifu wanapohitaji msaada chuoni. Watawalawakuu wa chuo wasisitize matumizi ya lugha sanifu ya Kiswahili ili kudumisha lugha hiyo hata katika maandishi. Matbaa yanayochapisha magazeti chuoni yachapishe magazeti mengi ya Kiswahili. Kulipendekezwa na watafitiwa kuwakuwe na hati nyingi zinazoandikwa kwa Kiswahili na katika shughuli rasmi matumizi ya Kiswahili yasisitizwe na kuhusisha Kiswahili katika shughuli zote za chuo. Mtafitiwa mmoja alitoa rai kuwa alifikiri mambo hayo yalitokana na ukosefu wa mikakati mwafaka katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Hivyo, wakuu wa Chuo waweke mikakati ifaayo kupitia idara ya upangaji lugha hapa nchini Kenya ili kuwezesha Kiswahili kuimarika zaidi. Pia idara ya Kiswahili Chuo kikuu cha Nairobi ijaribu kubuni istilahi nyingi za Kiswahili za kutumiwa katika idara tofauti ambazo si za Kiswahili na kuhakikisha wamefuatilia katika uongozi wa chuo kuwa kuna vifaa vya kutosha vya kuimarisha Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Katika mahojiano wanaoomba kazi waruhusiwe kuandika barua rasmi kwa lugha ya Kiswahili. Mahojiano pia yaendeshwe kwa Kiswahili si kwa Kiingereza tu. Idara ambazo si za Kiswahili kama vile idara ya Anthropolojia, Saikolojia, Historia, Jiografia, Sosiolojia, Diplomasia na zingine ambazo hazitumii Kiswahili zihamasishwe kutumia Kiswahili katika mikutano yao. Kwa njia hii watawala watakuwa wanaingiana na Giles (1982) kwamba lazima wanajamii waitumie lugha yao kutekeleza shughuli mbalimbali na utamaduni wake ili iweze kukua. Giles (1982) anafafanua kuwa kukubali kutumia lugha katika miktadha tofautitofauti hukuza utamaduni wake na kufunga mipaka ya kuhamia kundi nje. Hali hii hutokeza mwachano wa makundi yanayohusika.

Kwa kuzingatia maswali ya Vinyago ya Hojaji - Likati tulitumia kauli tano ambazo zililenga kutambua mielekeo chanya na hasi ya watafitiwa kuhusu Kiswahili kikiwa lugha rasmi navilevile ya taifa. Mfano;



(ix) Wasimamizi wakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi wanafaa kufahamu Kiswahili.

1. Nakubaliana kabisa

2. Nakubaliana

3. Sikubaliani kabisa

4. Sikubaliani

5. Sina maoni


Swali la kwanza na la pili yalilenga kutambua wenye mielekeo chanya kuhusu hali ya Kiswahili saa hii hata baadaye. Swali la tatu na la nne yamelenga wale wenye mielekeo hasi. Swali la mwishoni nalo lilikuwa linajaribu kuwatambua wale wasio na mielekeo yoyote chanya au hasi. Kati ya waliojaza hojaji watafitiwa ishirini na saba walijibu na kurudisha hojaji.

<b>Kauli</b>	<b>Idadi</b>	<b>Asilimia</b>	<b>Digrii°</b>
<b>Nakubaliana kabisa</b>	10	37%	133°
<b>Nakubaliana</b>	9	33%	120°
<b>Sikubaliani kabisa</b>	3	11%	67°
<b>Sikubaliani</b>	5	19%	40°
<b>Sina maoni</b>	0	0%	0°
<b>Jumla</b>	27	100%	360°

Mielekeo ya asilimia sabini (70%) ya watafitiwa ilikuwa chanya huku mielekeo ya asilimia 30% ikiwa hasi. Hakuna mtafitiwa yeyote aliyeonyesha kutokuwa na msimamo. Waliokuwa na mielekeo chanya walieleza kuwa Kiswahili bila shaka ni lugha ya taifa na husaidia katika maongezi ya kawaida ya kila siku chuoni. Vilevile, walifafanua kuwa katika jamii ya wingilugha kama inavyodhihirika pale chuoni Nairobi, kufahamu Kiswahili hasa msamiati wake ni jambo la busara kwani huwaunganisha wahadhiri na wanafunzi pamoja na wasimamiziwakuu wao. Pia kwa

vile Kiswahili kilipewa hadhi ya kutekeleza majukumu rasmi kukifahamu na matumizi yake ni jambo zuri na la busara na hii ni kwa sababu za kijamii na kiuchumi chuoni na nje ya chuo.

Watafitiwa walioonyesha mielekeo hasi walieleza kuwa lugha moja inatosha kujieleza wakidai kuwa katika Chuo Kikuu cha Nairobi, kuna wahadhiri wa kutoka nje ya taifa la Kenya na Afrika Mashariki. Hivyo, kwa maelezo ya wasimamizi wakuu na wahadhiri kama hao si lazima wajue Kiswahili bora wana uwezo wa kujieleza kwa Kiingereza.



Hata hivyo walifafanua kuwa kufahamu Kiswahili cha kuongea katika shughuli za kawaida ni sawakwa sababu kuelewa kilecha kuandikia ripoti za chuo ni vigumu. Aidha inaweza kuchukua muda mwingikufahamu Kiswahilikwa upevu zaidi. Katika uchanganuzi wa data yetu inabainika kuwa wasimamizi waku wa Chuo Kikuu cha Nairobi hawakupendelea kuwa lazima wakifahamu Kiswahili. Walionyesha kwa kiasi kikubwa mielekeo hasi. Walipendelea Kiswahilikama lugha ya kawaida kutekeleza shughuli za kawaida kuliko wajibu rasmi. Kwa mujibu wa majibu ya mahojiano watafiti wawangependa kukifahamu Kiswahili sanifu lakini wakijaribu kukitumia inakuwa ni balaa kwao. Ukweli ni kwamba watafiti wawengi walikubali Kiswahili kitumiwe

chuoni lakini katika hali tumizi ya utendaji wa Kiswahili ni kinyume chake. Kulingana na Giles (1982) huu ni mwachano.

Katika matokeo ya swali hili wasimamizi wakuu wa Chuo Kikuu cha Nairobi walisema wanakubali ambapo wawili wakasema wanakubaliana kabisa, mmoja sikubali kabisa na watatu sikubali. Hii inaonyesha mwelekeo hasi wa matumizi ya Kiswahili chuoni kama lugha rasmi. Maelezo zaidi ni kama tulivyowasilisha matokeo hayo. Wanaokubaliana wanajitokeza kama kundi ndani na wasiokubaliana wanajitokeza kama kundi nje. Wanaokubaliana wana mielekeo chanya na wasiokubaliana wana mielekeo hasi. Hawa ndio wanaweza kuhamia lugha yao na kuacha utamaduni wao na kuhamia lugha na utamaduni wa wengine ambao ni kundi nje kwa mujibu wa Giles (1982). Wasiokubaliana wana mielekeo hasi kuhusu Kiswahili wanajitenga kama kundi maalum la hadhi ya juu na wanaokubaliana kundi la chini. Kundi hili ndilo linalopelekea Kiswahili kuonekana kama la hadhi ya chini na kupendekeza kitumiwe kama lugha ya taifa tu bali si kama lugha rasmi. Hali hii inayojitokeza kwa watafitiwa wetu ndiyo inayoelezwa na Giles (1982) kwamba kundi la chini likigudua mpaka uliopo baina yake na kundi jingine wanatafuta mitindo ambayo itawafanya kuwa sawa na wenzao kama inavyoonekana kwa wanaokubaliana na wasiokubaliana kati ya watafitiwa wetu.

#### **4.2. Athari za mielekeo ya watawala wakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa.**

Mielekeo huchangia namna watu huteua lugha Fulani na kuitumia. Mielekeo chanya husababisha kupendwa na kutumiwa kwa lugha kutekeleza majukumu rasmi na yasiyokuwa rasmi. Kiswahili kama lugha ya taifa, kimechukuliwa kwa njia chanya ambazo zimeibua mielekeo chanya kwa kupendwa na watafitiwa wetu. Zaidi ya asilimia 60% ya watafitiwa wetu walieleza kuwa Kiswahili kama lugha ya taifa wanakipenda kwa sababu kinavunja ukabila nchini Kenya kwa kuwa kinatumika na kila mtu. Katika mahusiano ya watu ya kila siku Kiswahili ni lugha ambayo watu hutumia kutongoza. Kwa shughuli za ajira na kazi, Kiswahili ni chombo cha ajira ambapo watu wameajiriwa kukifunza, kuchapicha vitabu na vyombo vya habari kupeperushia habari. Wengi waliosema haya kuhusiana na Kiswahili kama lugha ya taifa ni wahadhiri wa idara ya lugha ambao walipenda sana wawe ni wahadhiri wa Kiswahili.

Kiswahili kimechukua nafasi ya utangamano wa kitaifa na katika usafiri. Vyeti vinavyohusu masuala ya Kitaifa huandikwa kwa Kiswahili na Kiingereza na kwa hivyo watu wanakichukulia

Kiingereza na Kiswahili kama lugha ambazo ziko sambamba katika hali moja kinyume lugha za Kienyeji kama vile Kimeru hali ambayo inaibua makutano na mwachano.Hizi athari za mielekeo chanya. Kutokana na maelezo ya watafitiwa wetu Kiswahili hutumiwa katika utangamano wa Kitaifa,kuendesha shughuli za chuo Kikuu cha Nairobi.Haya ni matokeo ya athari chanya.Kiswahili kimetokea kuwa lugha rahisi kwa kuwa ni lugha ya Kibantu na asilimia ya juu zaidi ya watawala wakuu na wahadhiri ni wabantu.Kiswahili ni lugha iliyoenea kote nchini Kenya na kwa hiyo inavunja mipaka ya kimawasiliano na kuwa lugha inayojulikana na yeyote yule hata hakwenda shule ambapo suala la kufahamu kiswahi na kutokwend shule ni muhimu sana.Haya yote athari chanya zinazotokana na matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa kwa watawala wakuu na wahadhiri wa chuo kikuu cha Nairobi.

Pasi na mielekeo chanya,watafitiwa wetu walieleza athari hasi kuhusu matumizi ya Kiswahili katika mianda rasmi.Kwa mujibu wa maelezo ya watafitiwa, Kiswahili kama lugha rasmi kimebakia nyuma katika utekelezaji wa majukumu rasmi chuonikwani kumbukumbu za mikutano ya Chuo Kikuu cha Nairobi hunukuliwa kisha kuhifadhiwa kwa kiingereza na pale Kiswahili kinapojitokeza hujitokeza ja nukuu zilizotajwa na wasemaji mikutanoni.Katika idara za chuo Kikuu cha Nairobi isipokuwa idara ya Kiswahili hotuba huandikwa na kusomwa kwa lugha ya Kiingereza na za Kiswahili hutolewa kama tafsiri za baadaye.Hizi ni athari hasi kwa matumizi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.Katika mahojiano na watafitiwa walieleza kuwa Kiswahili hakitumiki katika mianda rasmi kutekeleza shughuli rasmi chuoni kama inavyopaswa kwa mujibu wa katiba ya Kenya ya 2010 ambapo Kiswahili ni lugha rasmi ya Kwanza Kenya kama vile vyeti vya shahada.Hii ni ishara tosha kwamba kinachodokezwa katika hali hii ni athari hasi dhidi ya Kiswahili

Watafitiwa walisema kuwa toka taifa la Kenya lijinyakulie uhuruKiswahili hakijapewa nafasi na hizi ni athari hasi.Watafitiwa vile vile walionyesha kwamba hadhi ya Kiswahili kama lugha rasmi haijatambuliwa katika chuo Kikuu cha Nairobi.Kama tulivyoeleza katika matokeo ya utafiti,watafitiwa walishindwa kujieleza kwa Kiswahili sanifu na hiyo wanabakia kutumia Kiswahivyo ovyo na cha kubabaisha huku wakiibua mielekeo hasi ambayo inapelekea kutokuwa na wataalamu wengi waliojitokeza kuandika na kusoma maandishi mengi ya magazeti,vitabu na majarida ya Kiswahili.Fauka ya hayo,asilimia kumi ya watafitiwa walieleza kuwa kuna uwezekano kwamba katika kizazi kijacho kitachukia Kiswahili na kukumbatia Kiingereza kama lugha rasmi

na hizi ni athari ambazo ni hasi kwa lugha ya Kiswahili kutokana na historia pamoja na utamadui wa Chuo Kikuu Cha Nairobi nilichokitafiti. Hii ni kwa sababu hii ni asilimia dogo sana ikilinganishwa na wahojiwa tuliowahoji katika ujumla wao.

Kwa mujibu wa maelezo ya watafitiwa wetu kuna uwezekano wa kufa kwa Kiswahili kama lugha rasmi katika Chuo Kikuu cha Nairobi katika kizazi kijacho lao kama tahadhari hazikuchukuliwa. Kauli hii inakubaliana na ile ya nabea (2009) aliyesema kuwa japo Kiswahili kina wazungumzaji wengi katika Taifa katika shughuli rasmi huwa hakitumiwi bali watu wengi hukitumia Kiingereza. Kutokana na athari hizi hasi Kiswahili kina changamoto nyingi ambazo zinazuia maendeleo na utendakazi wake kama lugha rasmi katika Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Kama anavyoeleza Giles (1982) kwamba ili kundi nje lidumishe hadhi yake lazima liwape kundi la ndani nafasi kujiunga nao. Hali hii inajitokeza kwa wenye mielekeo chanya inayopelekea athari chanya. Aidha Giles (1982) anaeleza uwepo wa kundi ndani kutetea hadhi ya lugha yao. Katika Chuo Kikuu cha Nairobi wadau wenye mielekeo chanya ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa wanajukumu la kutetea Kiswahili katika utekelezaji majukumu rasmi. Hili ndilo litabadilisha mielekeo hasi kuwa na athari chanya. Athari hasi zimetokana na maswala ya kupendelewa kwa lugha za kigeni kama vile Kiingereza katika mazingira rasmi. Giles (1982) anasema kuwa mapendeleo ya lugha moja katika matumizi yanawezakuibua mielekeo na mipaka inayoibua kundi ndani na kundi nje kama hadhi ya juu na ya chini. Haya yanadhihirika kwa watawalawakuu wa Chuo Kikuu cha Nairobi kupendelea lugha moja na nkupuuza Kiswahili kama lugha rasmi katika mianda rasmi kuttekeleza shughuli rasmi hali ambayo imeibua athari hasi kwa Kiswahili kama lugha rasmi.

### **4.3 Hitimisho**

Tumejadili maswala yanayosababisha mielekeo dhidi ya Kiswahili na athari za mielekeo ya watawala wakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi kama lugha rasmi na ya taifa katika sura hii. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, Kiswahili kama lugha rasmi kimetingwa na maswala ya kiuchumi, kijamii, kiisimu na lugha rasmi ya Kiingereza ambayo yanaonekana kuibua mielekeo chanya dhidi ya Kiswahili kama lugha ya taifa. Kihistoria kile kilichoonekana kama kizuizi kwa Kiswahili ni lugha zingine kama vile Kiingereza ambacho kilichukuliwa kama lugha ya kuwapa watu elimu bora, ajira, kupanua na kuinua uchumi na kuwapa watu hadhi ya juu. Matumizi Kiswahili kama lugha ya taifa yaliungwa mkono kwa asilimia zaidi ya 80% ya Watafitiwa wetu.

Mapendeleo ya Kiswahili, kwa mujibu wa watafitiwa, ni kwa maana ya Kiswahili kuwakama lugha ya kujitambulisha na kujihusisha baina ya wahadhiri na wanafunzi na wasimamizi wakuu wao chuoni na wahadhiri na wanafunzi wa vyuo, mataifa jirani kama Tanzania, Uganda na Rwanda kunakofunzwa Kiswahili. Hizi ni athari chanya kutoka kwa watafitiwa kuhusiana na namna Kiswahili kinavyotumiwa kama lugha ya taifa. Mielekeo hasi imedhirisha athari hasi kuhusiana na matumizi ya Kiswahili kama vile kutofaulu kutekeleza wajibu wa lugha rasmi kama kinavyotarajiwa, kufifia kwa kizazi kijacho na mengineyo kama tulivyoeleza katika sehemu ya athari za mielekeo katika utafiti huu.

## SURA YA TANO

### 5.0 Muhtasari, Hitimisho na Mapendekezo

#### 5.1 Utangulizi

Utafiti wetu umetafiti mielekeo ya wahadhiri na watawalawakuu wa Chuo Kikuu cha Nairobi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa na athari zake. Tuliatafiti maswala yanayosababisha mielekeo ya watawalawakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa na athari zake. Kiini kilikuwa kubaini hali ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi sasa na hata baadaye kama lugha rasmi na ya taifa. Katika utafiti wetu tulipata data msingi kutoka kwa wakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi kutoka idara za isimu, lugha na maswasiliano za bewa kuu la Chuo Kikuu cha Nairobi. Hatukutafiti wakuu na walimu wa idara ya Kiswahili kwa sababu tulionelea kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kupata mielekeo chanya kwa wakuu na wahadhiri wa idara hiyo. Tuliutumia mbinu ya mahojiano, hojaji na utazamaji wa watafiti wakatika ukusanyaji wa data. Pia tulitumia nadharia ya makutano na mwachano ya Giles (1982) kuchanganua data yetua. Kulingana na mihimili ya Nadharia hii watu wanapokuja pamoja na kundi moja linaacha kutumia lugha yake na kuhamia lugha ya kundi jingine kujitambulisha nayo kwa sababu ya kuiona lugha ya wengine kama lugha bora kuliko yao huwa kumetokea makutano na ikitokea kuwa kila kundi linaendeleza shughuli za kila siku kwa lugha yao na kujitambulisha nayo na kuhifadhi utamaduni wao bila kupendelea ya wezao basi huwa kumetokea mwachano. Mihimili hii huwa na kundi ndani na kundi nje. Matokeo yameonyeshwa kama inavyodhihirika katika muhtasari wetu.

Katika sura hii tumejadili changamoto za utafiti, mapendekezo na mahitimisho.

#### 5.2 Muhtasari wa utafiti

Utafiti huu una sura tano. Vipengele vilivyotafitiwa vya kimsingi vimejadiliwa katika sura ya kwanza. Vipengele hivyo vilikuwa usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, misingi ya Kinadharia na mbinu za utafiti.

Katika sura ya pili, tumejadili historia ya mielekeo ya Kiswahili nchini Kenya Wakati wa uhuru, wakati wa Kikoloni na baada ya Uhuru tukijikita na namna Kiswahili kilivyochukuliwa na kutumiwa na vyombo vya habari, siasa na katika sekta ya elimu.

Katika sura ya tatu, tumechanganua matokeo yaliyotokana na utafiti huu huku vigezo vya umri na jinsia,viwango vya elimu kwa walengwa wetu vikizingatiwa.Katika uchanganuzi wa data tumebaini kuwa kuna mieleko chanya na hasi kwa wakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi.Pia wana mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kama lugha ya taifa.Kwa upande mwingine, zaidi ya asilimia sabini na tano ya watawala wakuu ina mielekeo hasi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi.Hivyo utendakazi wa Kiswahili kama lugha rasmi katika Chuo Kikuu cha Nairobi haupo.

Katika sura ya nne, maswala yaliyosababisha mielekeo ya watafitiwa kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa na athari zake zimejadiliwa. Matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa maswala yanayosababisha Mielekeo chanya ya Kiswahili ni masiala ya Kijamii yanayotokana na majukumu kinayotekeleza kama lugha ya taifa ya kuwaunganisha Wananchi,kuendeleza biashara,kutambulisha taifa na kadhalika.Mielekwo hasi ya Kiswahili nayo ikisababishwa na maswala ya Kiisimu,Kihistoria na ajira au kazi bora.Swala kuu lililotinga Kiswahili katika utekelezaji wa majukumu rasmi ni Kiingereza kwa kuchukuliwa kama lugha ya upataji ajira bora,elimu na kuwatia wazungumzaji wake katika hadhi ya juu zaidi kuliko wazungunzaji wa lugha zingine.Hata hivyo walipendekeza mikakati bora ibuniwe na Chuo Kikuu cha Nairobi ili kukipa Kiswahili nafasi yake kama lugha rasmi.

### **5.3 Changamoto za utafiti**

Tulikumbwa na changamoto nyingi katika utafiti huu. Mathalani, baadhi ya watawalawakuu wa Chuo hawakuwa tayari kutujazia hojaji. Kunao walikuwa wametingika katika shughuli za Chuoni kama mikutano ambayo iliwanyima nafasi ya kuhojiwa.

Wengine walikosa wakati wakujaza hojaji na kwa sababu hiyo wakachukua siku nyingi zaidi ya wiki kurundisha hojaji.Wahadhiri wengine walikuwa likizoni.Kuwapata baadhi yao idarani haikuwa rahisi.Wengi wao walishindwa kutoa maelezo kwa Kiswahili ikabidi watolee maelezo ya mahojiano kwa Kiingereza hivyo tukachukua muda kutafsiri hojaji na maelezo tuliyonasa kwa Kiingereza.Asilimia kubwa ya watafitiwa ilipendekeza kujaza hojaji za Kiingereza na hili pia likatulazimu kuchukua muda mwingi kuzitafsiri.



#### **5.4 Mahitimisho**

Tukihitimisha tunaweza kusema kwamba matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa, watafitiwa wetu: Watawala wakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi wana mielekeo kubalifu ambayo ni chanya kukihusu kiswahili kama lugha ya kitaifa na mielekeo hasi kama lugha rasmi hasa katika matumizi yake kutekeleza majukumu rasmi katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Waliokichukulia kuwa ni vigumu kukitumia katika Ofisi hasa Kiswahili sanifu walikuwa na mielekeo hasi. Japo wengi walionyesha mielekeo chanya ni kwa kwa kusema tu lakini utendaji wa Kiswahili kama lugha rasmi kama vile kuandika barua rasmi, kuhoji watu wanaoomba kazi kwa Kiswahili na utendakazi wa Kiswahili Chuoni haupo. Mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kama lugha ya taifa imetokana na historia ya kuwaunganisha Wakenya kwa jumla, kutumika hata katika miktadha ya nje ya chuo hasa katika mawasiliano ya kila siku ya watawalawakuu, wahadhiri na wanafunzi chuoni kwa jumla.

Baadhi ya watafitiwa walipendekeza kubuniwe kamati ya kushughulikia namna Kiingereza na Kiswahili kama lugha rasmi zitakuwa zinatumiwa Chuoni. Kanuni zitungwe zitakazoongiza matumizi ya lugha rasmi kutekeleza majukumu rasmi Chuoni. Vitabu vingi vya Kiswahili vichapishwe hasa vya kutafsiri baadhi ya misamiati ya Kiswahili ikilenga shughuli za idara katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Suala la Kiswahili katika utekelezaji wa majukumu rasmi ni mtajo uliokubaliwa tu bila kutiliwa mkazo Chuoni. Watafitiwa wanajua Kiswahili ni lugha rasmi lakini bado haijaanza kutumika. Hivyo urasmi wa Kiswahili Chuoni haujatambuliwa.

Tumetambua kuwa, maswala ya Kiisimu ndiyo yaliyokiangamiza Kiswahili kutotekeleza majukumu rasmi huku yakijenga na kujuza Kiingereza kutekeleza majukumu hayo. Maswala ya Kiuchumi, ajira na biashara yanayofanywa na watawalawakuu na wahadhiri nje ya Chuo yamepelekea Kiingereza kupewa hadhi kubwa kuliko Kiswahili na kukwamiza Kiswahili katika utekelezaji wa majukumu rasmi Chuoni. Hili lilidhihirika pale ambapo katika mikutano lugha iliyotumiwa ni Kiingereza. Kiswahili kilitumika katika mikutano hiyo kupunga hewa baada ya hoja iliyotolewa kwa kiingereza.

Darasani lugha iliyotumiwa kufunza kwa mujibu wa watafitiwa ni Kiingereza na baada ya darasa wakuu na wahadhiri walitangamana kwa kusemezana kwa kutumia Kiswahili ambacho si

sanifu. Kwa sababu hii hatua za dharura zinahitajika zichukuliwe kukwamua Kiswahili kama lugha rasmi katika Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kuagiza wakuu wanaohusika na upangaji wa lugha na utoaji maamuzi ya matumizi ya lugha ili tuondoe shida ya kuondolewa kwa idara ya Kiswahili chuoni kama ilivyotendeka hapo awali. Kwa ujumla matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi kama lugha rasmi hayana mashiko katika utendakazi wa shughuli rasmi na katika miktadha rasmi bali hutumika kama lugha ya kawaida.

## **5.5 Mapendekezo**

Baada ya uchanganuzi wa matokeo ya utafiti huu tumebaini kwamba, japo kuna watawalawakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi walionyeshwa mielekeo chanya kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa, utendakazi wa lugha hiyo kama lugha rasmi haujatambuliwa. Kiswahili hakijatambuliwa katika utendakaji wa majukumu rasmi Chuoni. Aidha, walioonyesha mielekeo chanya ni kwa sababu imesemekana hivyo katika katiba ya Kenya ya 2010. Hivyo tunapendekeza watawala wakuu wa Chuo Kikuu cha Nairobi wabuni mikakati ya kutekeleza majukumu rasmi kwa Kiswahili katika Idara ambazo si za Kiswahili Chuoni.

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, tunapendekeza kubuniwe tume au baraza la utetezi wa maendeleo ya Kiswahili Chuoni lenye watetezi imara wa Kiswahili ili kuondoa suala la kuondolewa kwa Kiswahili kama mojawapo ya idara za Chuo Kikuu cha Nairobi.

Chuo Kikuu cha Nairobi kiwe kinachapisha vitabu vya Kiswahili sio vya Kiingereza pekee. Kukiwezekana chuo kijenge matbaa ya kuchapisha vitabu vya Kiswahili na katika matbaa hiyo kuwe na Wahariri wa miswada ya Kiswahili.

Pasi na hayo tunapendekeza kuwa Watawala wakuu wa Chuo Kikuu cha Nairobi wakipe Kiswahili nafasi sawa na Kiingereza katika mianda rasmi ili kutekeleza majukumu rasmi. Hali hii itaondoa maonevu hasa wakati wa kuendeleza mikutano chuoni, shughuli za mikutano ya hadhara ya wanafunzi na shughuli za maadhimisho kutolea hotuba kwa Kiswahili ili kukuza na kukipa Kiswahili mizizi ya kukua. Tunapendekeza Chuo Kikuu cha Nairobi kukubali Kiswahili kitumike kama lugha ya kuendeleza mahojiano na kuandikia barua rasmi na stakabadhi zingine za Chuo kama vile vyeti vya wanafunzi, vitambulisho vya wanafunzi na kutumia Kiswahili kutoa habari za matangazo ya Chuoni kwa wavuti, tovuti na kwa mitandao ya chuo kwa jumla bila kupendelea lugha rasmi ya Kiingereza.

Vifaa vya kutafsiri maneno ya Kiswahili vishughulikiwe na chuo. Hili litasaidia kupata vitabu vingi vilivyotafsiriwa kwa Kiswahili ili kupata msamiati wa kutosha na istilahi za kutumiwa katika Idara zote ambazo si za Kiswahili.

Kutokana na changamoto za uhaba wa hela za kutosha na wakati, tuliubana utafiti wetu kwa wakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi. Chuo hiki kina wahadhiri na watawala wakuu wa makabila tofauti na wengine kutoka mataifa ya nje ya bara la Afrika ambako lugha zingine pasii na Kiswahili huzungumzwa. Ili kukipa Kiswahili urasmi wake katika utendaji wa majukumu rasmi, washikadau wengine wa sera ya lugha nchini wahusishwe ili kusaidia idara ya Kiswahili kufanikisha na kutoa mielekeo hasi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kwa sababu hizi tunapendekeza tafiti zingine zaidi zifanywe kuhusiana na masuala yafuatayo:

- (i). Utafiti unaohusisha wanafunzi wa vyuo vikuu kuipima mielekeo yao kuhusiana na suala la lugha katika vyuo vikuu nchini Kenya.
- (ii). Utafiti pia ufanywe ukihusisha watawala wakuu wa vyuo vikuu ili kujua ukubalifu wao kuhusu matumizi ya Kiswahili katika kufunzia masomo mengine vyuoni.
- (iii). Utafiti ufanywe kwa wakuu wa sera za lugha vyuoni kubaini mielekeo yao kuhusu matumizi ya Kiswahili kutumiwa kuandikia stakabadhii zinazotolewa Chuoni kama vitambulisho, vyeti na vitabu vya wanaohitimu vyuoni, kadi za mitihani na kuandika barua rasmi chuoni.
- (iv). Nchi ya Kenya inatambua lugha Ishara na Breli kutumiwa na Wakenya. Hivyo utafiti ufanywe kuhusu hali ya lugha Ishara na Breli katika Vyuo Vikuu nchini Kenya.

## **MAREJELEO**

Abdulaziz, M.H. (1982) *Patterns of Language Acquisition and use in Kenya: Rural-Urban Differences*. Katika Polome, E Mhr. International Journal of the society of Language Vol 34

- Adoyo, P.O (200). Emergent Approaches towards Sign Bilingualism in Deaf Education in Kenya.Stichproben. Wiener Zeitschrift Fur Kristche African Studen
- Ali, J.N. (2011). Changamoto zinazokumba mawasiliano ya kiafisi kwa kutumia Kiswahili kama lugha rasmi. Mradi wa shahada ya kwanza. Chuo kikuu cha katoliki cha Afrika Mashariki
- Chimerah, R. (1998) Kiswahili Past, Present and Future Horizons.Nairobi.Nairobi University Press.
- Chiraghdin, s.na Mnyampala, M. (1977). Historia ya Kiswahili.Nairobi University Press
- Fink, T.K. (2005). Attitudes towards Language in Nairobi.Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Pittsburgh.
- Gardner, R.C. na Lambert, W.E (1959). The Social-Psychological Theory of Second Language (L2)
- Gorman, T.B (1974) The Development of Language Policy in Kenya with Particular Reference.
- Habwe, J.et al (2010).Darubini ya Isimujamii kwa Shule na Vyuo.Nairobi. Phoenix
- Iribemwangi, P.na Mukhwana, A. (2011). Isimujamii.Nairobi; Focus
- Jones, J.M (2012).The Effects Language on Kengan Stakeholder Involvement.
- King'ei, K. (2010) Misingi ya Isimujamii.Dar Es Salaam TUKI
- Lambert, W.E. Hodson, R.Gardner.R.C.na Fillenbaum, S. (1960). Evaluation Reactions to Spoken Languages.Journal of Abnomal and Social Psychology:60(1) 44-51
- Mathoko, P.M. (2007). Isimujamii; Misingi na Nadharia. Njigua Books.Nairobi.
- Mazrui, A. Mazrui, M. (1995) Swahili State and Society: The Political Economy of an African Language. East African Education Publishers
- Mazrui, A.M. (1978). The Religious Factor in Language Nationalism: The case of Kiswahili in Kenya.Katika Studies in Africa Linguistics.Vol.9.NO. 2 178 University of California
- Mbaabu, I. (1978). Kiswahili Lugha ya Taifa.Kenya Literature Bureau

- Mbaabu, I. (1991) Historia ya usanifishaji wa Kiswahili: Nairobi.Longman Kenya
- Mbaabu, I. (1996).Language Policy in East Africa.Educational Research and Publication. (ERAP)
- Mirianga, R.K. (2014). Mielekeo ya Walimu wa Shule za Msingi Kuhusu Suala la Lugha Kama Linavyoelezwa Katika Katiba ya Kenya.Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi Kenya.
- Mohochi, S. (2011).Mielekeo ya Wasomi wa Kiswahili na Viongozi wa Afrika Mashariki Kuhusu Lugha ya Kiswahili.Swahili Forum.18:24-36
- Mugenda, O.M. na Mugenda, A.G. (1999) Research methods: Quantitative and qualitative Approaches.Africa center for Technology Studies.Nairobi
- Mugenda, O.M Na Mugenda, A.G. (1990). Research Methods; Qualitative and Quantitative Approaches.Nairobi act Press.
- Mukhwana, A. (2008).Language Attitudes in Urban Kenya. A case Study of Nairobi, Mombasa and Kisumu, PHD thesis, Nairobi University
- Nyandwaro, L.K. (2015). Mielekeo ya Wafanyakazi Kuhusu Kiswahilikama Lugha Rasmi Katika Wizara za Serikali Nchini Kenya, Tasnifu ya uzamili Chuo kikuu cha Kenyatta.
- TUKI (1990) Kamusi sanifu ya Lugha na Isimu.Dar Es Salaam.University of Dar Es Salaam
- Whitely, W.H. (1974).Language in Kenya.Nairobi.Oxford University Press.
- Whitley, W.H (1969) Swahili: The Rise of a National Language.OUP, 1969 Language in Kenya OUP Nairobi



**UNIVERSITY OF NAIROBI**  
**OFFICE OF ASSOCIATE VICE-CHANCELLOR**  
 (Research, Innovation and Enterprise)

P.O. Box 29548/08  
 Nairobi, Kenya  
 Website: [www.uoi.ac.ke](http://www.uoi.ac.ke)

TEL: +254 20 770 1111  
 Email: [uoi@uoi.ac.ke](mailto:uoi@uoi.ac.ke)

UON/RIE/RS/Wd/XX

July 27, 2022

Mr. Murea Wilson Mbas  
 P. O. Box 117-50667  
 MKINDURI-MURU  
 Tel: 0727282081

Dear Mr. Murea

**PERMISSION TO COLLECT DATA**

I refer to your request to conduct research at the University of Nairobi for your project entitled: *"Mitekezo ya Wakazi wa Wakadiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi kuhusu Kivutiki Kwaot Light Rasmii na ya Tinja na Akari Zake."*

I write to inform you that your request has been approved.

You are however required to share the findings of your study with the University of Nairobi by depositing a copy of your findings with the Director Library & Information Services on completion of your study.

Yours Sincerely,

**PROF. M. JESANG HUTCHINSON**  
 ASSOCIATE VICE-CHANCELLOR (AG-)  
 (RESEARCH, INNOVATION AND ENTERPRISE)  
 AND  
 PROFESSOR OF HORTICULTURE

Copy to: Director, Library and Information Services

202207



REPUBLIC OF KENYA



NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 798037

Date of Issue: 25/July/2022

RESEARCH LICENSE



This is to Certify that Mr. MUREA WILSON MBASI of University of Nairobi, has been licensed to conduct research in Nairobi on the topic: MIELEKEO YA WAKUU NA WAHADHIRI WA CHUO KIKUU CHA NAIROBI KUHUSU KISWAHILI KAMA LUGHA RASMI NA YA TAIFA NA ATHARI ZAKE. for the period ending : 25/July/2023.

License No: NACOSTI/P/22/19203

798037

Applicant Identification Number

W. Mbasi

Director General

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code



NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

## **HOJAJI YA UTAFITI KWA LUGHA YA KISWAHILI**

### **HOJAJI YA UTAFITI**

Mimi ni mwanafunzi wa Shahada ya Uzamili katika Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Nimekuja kuomba msaada wako katika kujaza hojaji inayohusu masomo yangu.

Naomba nikuhakikishie kuwa majibu utakayonipa yatatumika kwa ajili ya utafiti huu pekee na wala si kwa shughuli nyingine yoyote ile.

### **MIELEKEO YA WAHADHIRI WA CHUO KIKUU CHA NAIROBI KUHUSU**

#### **KISWAHILI KAMA LUGHA RASMI NA YA TAIFA NCHINI KENYA**

Utafiti huu unakusudia kuchunguza mielekeo ya watawala wakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa na athari zake. Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kuwasaidia wapangaji lugha kupanga na kukipa Kiswahili nafasi yake na kujua iwapo lugha hupangwa au hujipanga yenyewe.

Majibu yako kwa maswali yafuatayo yatatumiwa kwa shughuli ya kiutafiti na yatakuwa ya siri. Kwa hivyo usiandike jina lako kwenye hojaji tafadhali.

### **SEHEMU A HABARI ZA KIMSINGI KUHUSU MTAFITIWA**

(i) Jinsia: Kike..... Kiume.....

( Tia alama ya X kwenye jibu ulilochagua)

(ii) Umri.....

( Chagua kati ya a,b,c , d na e)

(a) Kati ya miaka 30 na 40

(b) Kati ya miaka 40 na 50

( c) Kati ya miaka 50 na 60

( d) zaidi ya miaka 60



(e)zaidi ya miaka 60

(iii) Kazi chuoni hapa (Tafadhali sema kama ni uhadhiri au usimamizi)

(iv) Idara ya.....

(v) Umefundisha kwa muda gani? (Tafadhali taja idadi ya miaka).....

(vi) Umekuwa katika ngazi ya uandamizi kama mtawala chuoni hapa kwa muda gani? (Tafadhali taja miaka).....

(vii) Eneo/nchi ya kuzaliwa .....

(viii) Taaluma inayoegemewa chuoni hapa .....

**SEHEMU YA B MASWALI KIDADISI CHA UTAFITI HASA**

(i) (a) Kiswahili ni lugha iliyopewa nafasi ya kutekeleza majukumu rasmi nchini Kenya. Kwa maoni yako Kiswahili kinaweza kutumiwa kufundishia masomo mengine chuoni hapa?( Sema ndio au la).

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako.....

(ii) Je, ungependa kutumia lugha gani unapowahutubia wanafunzi katika mikutano ya nje ya darasa?)

(Chagua moja kati ya a,b,c,d na e).

(a) Kiswahili

( b) Kiingereza

( c) Kichina

(d) Kikorea

( e) Kuchanganya lugha hizi zote

( iii) Toa sababu za jibu ulilochagua tafadhali .....

(iv) Maoni yako ni yapi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa nchini Kenya?

(v) Kwa maoni yako ,kuna manufaa ya Kiswahili kutumika kama lugha rasmi na ya taifa nchini Kenya?( Sema kama ni ndio au la).

( b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako.....

(vi) Kwa maoni yako, kuna manufaa ya Kiingereza kutumika kama lugha rasmi nchini Kenya?

Tafadhali eleza sababu za jibu lako .....

(vii) Kwa maoni yako, kuna uwezekano wa kutumia Kiswahili na Kiingereza kwa usambamba kama lugha mbili rasmi nchini Kenya katika vyuo vikuu?( Sema kama ni ndio au La).

Tafadhali eleza sababu za jibu lako .....

( viii) Katika upeo wa matumizi ya lugha zifuatazo unaweza kusemaje?

( Chagua mojawapo ya majibu hayo kwa kila lugha ; upeo wa chini,upeo wa kati na upeo wa juu)

( a) Kiswahili

( b) Kiingereza

( c) Kichina

( d ) Kikorea

(ix) Ni lugha gani unafikiri inampa mwanafunzi fursa nzuri zaidi ya kupata ajira nzuri katika siku zake za usoni nchini Kenya? .....

( b) Toa sababu za ni kwa nini unafikiria hivyo hasa kwa kurejelea hali za lugha katika mataifa unayoyafahamu .....

(x) Wewe kama mtu binafsi unayaonea fahari mazungumzo rasmi kwa kutumia lugha ya Kiingereza kuliko Kiswahili na lugha zingine kama Kichina na Kikorea.( Sema kama ni ndio au la)

( b)Tafadhali eleza sababu za jibu lako. ....

( xi) Wewe kama mtu binafsi unayaonea fahari mazungumzo rasmi kwa kutumia lugha ya Kiswahili kuliko Kiingereza.(Sema kama ni ndio au la)

( b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

( xii) Unayaonea fahari mazungumzo ya chuoni hapa kwa kutumia lugha ya Kichina na Kikorea kuliko Kiswahili na Kiingereza.( Sema ndio au la)

( b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

( xiii) Baina ya Kiingereza na Kiswahili, ungependa kutumia lugha ipi kutoa hotuba rasmi chuoni hapa?

( b) Tafadhali eleza sababu za jibu lako.

( xvi) Kuna manufaa katika kukuza,kutunza na kuendeleza matumizi ya lugha za kiasili kama vile Kiswahili .(Sema kama ni ndio au la).

(b) Tafadhali eleza sababu za jibu

lako.....

( c) Kwa maoni yako,serikali ya Kenya inaweza kutumia mbinu gani ili kuweza kukuza, kulinda na kustawisha matumizi ya lugha za kiasili za Wakenya?

(xvii) Ni muhimu kwa serikali kulinda na kustawisha matumizi ya lugha ishara ya Kenya, Breli na njia nyingine za mawasiliano na teknolojia zinazoweza kufikiriwa na watu wenye ulemavu .( Sema kama ni ndio au la)

(b) Eleza sababu za jibu lako.....

(c) Unafikiri serikali ya Kenya inaweza kustawisha matumizi ya lugha ishara ya Kenya na vilevile Breli ili kufikiwa na watu wenye changamoto za kimaumbile? Vipi?Tafadhali eleza.

(xviii) Kwa maoni yako ni akina nani kati ya watu wafuatao wanafaa kufunzwa matumizi ya lugha ishara ya Kenya na kwa nini? (pigia mstari kwenye jibu)

Wasiosikia pekee, wanaosikia pekee, wanaosikia na wasiosikia .....

(xix) Kwa maini yako, ni akina nani kati ya watu wafuatao wanafaa kufunzwa matumizi ya Breli na kwa nini?.(Pigia mstari kwenye jibu).....

(a) wasioona pekee,wanaoona pekee,wasioona na wanaoona .....

(b) Eleza sababu za jibu lako.....

(xx). Kwa maoni yako ,ni lugha gani imekoma kimsamiati nchini Kenya baina ya Kiswahili na Kiingereza ? .....

( b) Toa sababu za ni kwa nini unaishikilia kauli yako uliyoitoe hapo juu.....

Ninashukuru sana kwa muda ulionipa. Mchango wako umekuwa muhimu sana katika utafiti huu.

(xxi) Maswali ya vinyago

Tafadhali pigia mviringo (o) katika taarifa uliyopewa hapo chini ukionyesha kwamba ;

1. Ninakubaliana kabisa

2. Ninakubaliana

3. Sikubaliani kabisa

4. Sikubaliani.

5. Sina maoni.

(a) Kiswahili ni lugha inayostahili kutumika katika mawasiliano ya kila siku.

1    2    3        4        5

(b) Kiswahili hutumiwa sana na watu wenye viwango vya chini ya elimu.

1    2    3        4        5

(c) Viongozi wakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi wanastahili kufahamu na kutumia katika mawasiliano yao lugha ya Kiswahili.

1   2   3   4   5

(d) Ni vigumu kuzungumzia shughuli za Chuo Kikuu cha Nairobi kwa lugha ya Kiswahili?

1   2   3   4   5

(e) Kiswahili ni lugha iliyo na manufaa katika maisha ya watu wa Kenya kwa jumla.

1   2   3   4   5

## **HOJAJI YA UTAFITI KWA LUGHA YA KIINGEREZA**

### **RESEARCH QUESTIONNAIRE**

I am a M.A postgraduate student in Kiswahili Department at the University of Nairobi .i am kindly requesting for your assistance in filling in this questionnaire that concerns my studies.

Attitude of University of Nairobi administrators and lecturers towards Kiswahili as a national and official language

The aim of the study is to assist in the assessment of the university of Nairobi leaders and lectures attitude towards Kiswahili as a national and an official language.

It is expected that the research findings will help those who are concerned in language planning in Kenya to lay down appropriate strategies to control language situations and give Kiswahili its position as a national and an official language in Kenya.

The answers to the following questions will be used only for research purposes and will be treated as private and confidential. Please do not write your name on this questionnaire.

Please answer the following questions to the best of your knowledge.

#### **SECTION A**

(i) Gender. Male.... Female....

( Mark  on your answer.

(ii) Age...

( Choose either a b c or d)

(a) Between 30 and 40

( b) Between 40 and 50

( c) Between 50 and 60

(d) Above 60

(iii) Department? .....

(iv) For how long have you been teaching? .....

**SECTION B**

(i) Kiswahili has been given an official role in Kenya. In your own opinion, should Kiswahili be used as language of instruction in the university of Nairobi?

(Choose yes or no)

Please give reasons for your answer

(ii) Which language would you like to use when addressing students during meetings outside the classroom? (choose either a, b, c or d)

(a) Kiswahili (b) English (c) Chinese (d) Korean

Please give a reason for your answer.

(iii) What is your opinion about Kiswahili as a national and official language of Kenya provided in the Kenyan constitution?

(iv) In your opinion is there importance of using Kiswahili as a national and official language in Kenya? (Say yes or no)

Please give reason for your answer.

(v) In your opinion is the importance of using English as an official language in Kenya.

( Say yes or no).

Please give reason for your answer

( vi) What would you say about your frequency of use of the following languages.

( Choose either high, moderate or low).

(a) Kiswahili

( b) English

(c) China

(d) Korean

(vii) Which language do you think would contribute to a student getting a good employment in future?

Why?

(viii) I am proud of an official conversation when using English language rather than when i use Kiswahili (choose yes or no).

Please give reason for your answer.

(ix) i am proud of an official conversation when using Kiswahili language rather than when using English.( Choose yes or no)

Please give reason for your answer.

(x) am proud of a university conversation when using Korean or Chinese language rather than when using English or Kiswahili.( choose yes or no).

Please give a reason for your answer.

( xi) Between English and Kiswahili ,which language would you prefer when giving official speech?

Give a reason for your answer

(xii) In your opinion, what strategies can the Kenyan government use in order to promote, protect and develop the use of indigenous languages of Kenyan people?

(xiii) It is important for the Kenyan state to protect the development and use of the Kenyan sign language and braille and other communication networks available to people with disabilities.( Say yes or no).



Please give a reason for your answer.

(xiv) in your opinion ,in what ways can Kenyan state protect the development and use of the Kenyan sign language and braille in order to make them available to people with disability?

(xv) in your opinion ,who among the following people should be taught to use the Kenyan sign language.( Underline your answer)

The deaf only, the hearing only, both the deaf and the hearing

Please give a reason for your answer.

(xvi) In your opinion, who among the following people should be taught the use of Braille?( Underline your answer).

The blind only, the sighted only, both the blind and the sighted.

Please give reasons for your answer.

(xvii) In your opinion, which language between English and Kiswahili has more developed vocabulary?

Why?

### **HOJAJI KWA VIONGOZI WA CHUO**

Huu ni utafiti unaochunguza mielekeo ya watawala wakuu na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Naitobi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa nchini Kenya.

Tafadhali jibu maswali yote kwa kutoa majibu mwafaka,ukizingatia maswali uliyoulizwa. Habari nitakazozipokea kutoka kwa hojaji zitakuwa za siri mno

1. Jina la idara unayoongoza...

2. Jinsia (Tia alama kike... Kiume...

3. Tia alama kwenye umri wako

Kati ya miaka 30\_40 [ ]

Kati ya miaka 40\_ 50 [ ]

Kati ya miaka 50-60 [ ]

Zaidi ya miaka 60 [ ]

4. Umekuwa kiongozi kwa idara hii kwa miaka mingapi?

5. Katika idara yako,kuna lugha zipi zinazotumiwa katika mawasiliano?

6. Unapenda kutumia lugha ipi unapohutubu katika mkutano wa idara?

Kiingereza [ ] Kiswahili [ ] Kichina [ ] Kikorea [ ] kuchanganya lugha hizi zote [ ]

7. Una ufahamu wowote wa mielekeo dhidi ya Kiswahili miongoni mwa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili katikaidara yako humu chuoni?

8. Mwelekeo wako ni upi kuhusu Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa? Hasi ( ) chanya( )

Tafadhali toa sababu za,jibu lako.

9. Maoni yako ni yepi kuhusu mustakabali wa lugha ya Kiswahili Kenya?

10. Kwa maoni yako ,unafikiri hali ya Kiswahili itakuwaje hapo baadaye.

Nashukuru kwa muda ulionipa.Mchango wako umekuwa muhimu sana katika utafiti huu.

Ungependelea lugha ya Kiswahili itimiwe katikashughuli rasmi kenya kama kuandika barua rasmi? Ndio ( ) La ( )

Kwa nini?

Maranyingi watu ambao hawajaelimika katika nchi ndio hutumka kiswahili katika mazungumzo

1 2 3 4 5

Wanafunzi wana mielekeo ipi kuhusu kiswahili kamalugha rasmi na ya taifa?

Chanya ( ) Hasi ( )